# *Msiogope, Ni Mimi*

Ni vizuri sana kuwa hapa tena usiku wa leo. Ndio kwanza tuwe na wakati mzuri sana jana, nami nimekuwa nikiishi katika mazingira ya mkutano wa jana siku nzima leo. Kwa hiyo nina furaha sana kuwa katika ibada ya Bwana usiku wa leo.

2 Sasa, kukiweko na wengi sana wanaongojea, ama waliosimama, hasa, ambao ninapaswa kusema wamesimama, hasa, kwamba tunasikitika kwamba hatuna nafasi ya kutosha kuketi, lakini tunajua ya kwamba kama mkituvumilia kwa muda kidogo, Bwana hakika atawapa thawabu, natumaini atawapa. Nami nina hakika atawapa, kwa sababu Yeye daima huwapa thawabu walio na subira, na "Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya, nao watapaa juu kwa mbawa kama tai."

3 Sasa, siku chache zilizopita usiku, ama siku, nimekuwa tu nikihubiri, kwa namna fulani, kwenu, na kufanyiza mistari midogo ya kuita, na kadhalika, Kwa namna fulani ninaamini ninawiwa na wagonjwa usiku wa leo kuwaombea wagonjwa, kwa sababu kuna wengi sana wao hapa, nani niliwaambia hao wavulana wagawe kadi za maombi alasiri ya leo. Nadhani walifanya hivyo, ama je, waligawa? Je, waligawa? Hilo ni sawa, sawa. Tutaninii. . .(Asante, Ndugu Gene.) Tutawaita katika dakika chache tu.

4 Nilimwomba Ndugu Moore azungumze kwa niaba yangu, usiku wa leo, jambo pekee lingenibidi kufanya ni kuingia, kuwaombea wagonjwa. Ulifanya hivyo? Kuna mtu anayetaka kazi ya kunifuata, kuzungumza kwa niaba yangu? Loo, kote kote. . .Loo, jamani! Vema, mimi. . .

5 Leso hizi hapa zinazotumwa hapa juu kuombewa, sasa, tunaamini kwa uchaji kuombea vitambaa hivi. Sasa, tunakumbuka ya kwamba hili ni Fundisho la Biblia kuombea vitambaa hivi. Sasa, watu wengi huvipaka mafuta na kuvirudishia wagonjwa. Tunatuma maelfu yao kote ulimwenguni kwa mwezi. Na kama huna moja hapa ndani, kama ukiandikia tu ofisi yetu, mbona, hakika tutakutumia bila malipo, hakuna malipo kwa lolote tufanyalo.

6 Kwa hiyo, katika Biblia, kama mtanivumilia, ninaamini Kimaandiko, Paulo hakuviombea wala kuvitia mafuta, walichukua ktoka mwilini mwake. Ninaamini Paulo alikuwa wa Kimaandiko, sivyo? Mngetaka kujua mahali ninapowazia alitoa hilo? Eliya wakati mmoja, mtoto mchanga alipokufa, Eliya alimwambia Gehazi, "Chukua fimbo yangu, uende ukaiweke juu ya huyo mtoto."

7 Sasa, Eliya alijua ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa juu yake, na kila kitu alichogusa kilibarikiwa. Basi akasema,

"Chukua fimbo hii, ukaiweke juu ya huyo mtoto mchanga." Nafikiri hapo ndipo Paulo alipata wazo la kuweka . . . kuchukua leso na nguo kutoka mwilini mwake, kwa sababu nisingewazia kwamba Mtakatifu Paulo angefanya jambo lolote lisilo la kimaandiko. Kwa hiyo akatuma . . .

8 Sasa, tunatambua, ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali Yeye angali ni Yesu, mnaona, Yeye angali ni Mungu. Kwa hiyo Mungu, kwa kuwa hana upendeleo, anawatuma wachungaji wenu, na wainjilisti, na kadhalika, mpate kuwa na imani ile ile katika Mungu yeye yule ambaye Mtakatifu Paulo alimwakilisha. Na basi kama tuna huduma ile ile aliyokuwa nayo Mtakatifu Paulo, mambo yale yale yanatendeka katika huduma yetu, yanatukia, yaliyotukia katika mkutano wa Mtakatifu Paulo.

9 Sasa, kabla tu sisi, ama, usiku wa leo kabla hatujaanza kuwaombea wagonjwa, ni—ninataka kuweka mikono juu ya leso hizo na kuziombea. Mara nyingi . . . Nina picha, mnaona katika vitabu kule, kutoka Afrika Kusini ambako walikuwa, ninaamini, na magunia kumi na sita au kumi na manane yaliyojaa. Ibada ya usiku mmoja, makubwa tu kabisa, tunayaita, nadhani ni magunia ya turubai na yaliyoshindiliwa leso, na barua, na kadhalika. Ndipo mmoja wa waandishi wa habari akasema, "Ndugu Branham ni mshirikina sana, alikuwa akiombea vitambaa," leso.

10 Kwamba, hawayajui Maandiko, hivyo tu, wao ni watu wa kupendeza, ni kwamba tu hawaelewi. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, wote ni watu wazuri, lakini mara nyingi hawaelewi, kwa hiyo tunavumilia tu jambo hilo.

11 Kwa hiyo basi tunafurahia kuhudumu kwa njia yoyote. Sasa, kama ukiandikia Jeffersonville, waambie tu, itakuwa ni kitambaa nilichoombea. Siwezi kutuma leso, ni ghali sana kutuma maelfu ya hizo kwa mwezi, ninachukua utepe na kuukatakata na kuombea tepe hizi, na halafu dada fulani huko Illinois ananitengenezea vitambaa vidogo namna *hiyo*, si ghali sana, loo, nafikiri, ninasahau wanacholipa, mia moja, kwavyo. Nasi tunavichukua kwa yale masanduku makubwa mno, nami ninavichukua hivyo na kuviombea. Halafu basi kuna barua iliyoandikwa, tuna mnyororo mduara ulioizunguka dunia, dunia nzima imezungukwa na huu. Tuna miujiza mingi inayofanywa na vitambaa hivyo kuliko tuliyo nayo moja kwa moja mkutanoni, kwa sababu tunawafikia watu wengi zaidi.

12 Ninapenda kusimulia hili, ninajua linachukua muda wenu mwingi, lakini siku chache, loo, sio siku chache, michache, yapata miaka miwili iliyopita, kulikuwa na kimoja kilichotumwa Ujerumani, nacho kitambaa kimeandikwa, "Kama mchungaji we—wenu ni mwaminio, mwalike, kama umefanya dhambi yoyote, iungame, rekebisha kila kitu, Mungu hataponya, ila tu chini ya masharti." Mnaona? "Kwa hiyo

mwalike mchungaji wako, na kama umefanya kosa lolote, liungame, Biblia ilisema, 'Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kwa maana kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.'"

13 Nami nasema, "Kama nanii wako . . . Kama huna mchungaji anayeamini katika uponyaji, labda una jirani anayeamini katika uponyaji, mshiriki fulani wa kanisa, mtu fulani unayeweza kuzungumza naye na—na kumwambia siri zako."

14 Basi maskini mwanamke huyu wa Kijerumani akawaita wanawake jirani, naye akasema, "Kama nimefanya kosa lolote, niko tayari kulisahihisha, sijui lolote kulihusu." Alikuwa mlemavu kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka ishirini na kitu. Kwa hiyo wakaomba na kuitoa ile leso kutoka kwenye barua, wakaiweka juu ya maskini mwanamke huyo Mjerumani. Nyuma ya ukurasa kulikuwa na mahali ambapo wanatoa tafsiri ya ushuhuda wake, akasema, "Sasa, ewe ibilisi wa kale, umekuwa ndani yangu muda mrefu vya kutosha, kwa hiyo toka uende." Akasimama tu kutoka kwenye kiti cha magurudumu, na akaenda zake akitembea.

15 Sasa, ni rahisi tu hivyo. Naam, bwana. "Ewe mzee ibilisi, umenishikilia muda mrefu vya kutosha, sasa toka ndani yangu," ndipo akasimama tu papo hapo, akatoka akitembea. Sasa, hivyo ndivyo tu ilivyo rahisi.

16 Mimi na Ndugu Jack Moore kwenye, moja ya misheni zetu za kwanza kwenda magharibi, sijaliwazia hili kwa muda mrefu, tulikuwa tukiwaombea Wahindi huko San Carlos. [Ndugu Jack anasema, "Nilikuwa nikiwazia jambo lilo hilo."—Mh.] Naam. Ulikuwa ukiliwazia? Vema, labda Bwana ananitaka niseme jambo fulani kulihusu basi. Tulikuwa huko chini pamoja na Wahispania, mara ya kwanza niliyopata kuwaombea Wahindi, basi kulikuwa na mlevi sugu, na mwenye kifua kikuu akaja mkutanoni huko Phoenix, kwenye Ukumbi wa Shule ya Upili ya Byrd.

17 Ndipo nilipowaona wakiwaleta hao Wahindi jukwaani, moyo wangu daima uliwahurumia Wahindi, kwa vyovyote vile. Vema, nafikiri walidhulumiwa kutokana na hali hii ya Marekani. Kwa hiyo basi, ili kwamba, nilimwomba Bwana kama angewaponya hao Wahindi wawili, na kulifanya hakika awaponye, basi ningerudi kwenye hiyo hifadhi. Kabla sijafika California kulikuwa na mtu pale aliyenijulisha ya kwamba wote wawili waliponywa.

18 Kwa hiyo ilitubidi kurudi kule kwenye hifadhi, nami nakumbuka nikienda kule, na kuzungumza na hao Wahindi, hao Waapache, watu wakubwa mno, wenye nguvu pale wameketi huko, kila mahali. Nami nikasema, "Sasa, ninajua jinsi hapana shaka mnajisikia." Nikasema, "Nafikiri ni kosa kutuma mabilioni ya dola nchi za ng'ambo wapate kutengeneza ndege,

na kutengeneza mabomu, kisha wanarudi na kutulipua nayo, hiyo ni kweli, wakati maelfu ya hawa Wahindi wanakufa kwa njaa kila mwaka humu mbugani."

19 Ni—ni doa kwenye bendera yetu kufanya jambo kama hilo. Hata hivyo, nchi hii ni mali yao, tuliwasukuma nyuma tu. Tungewazia nini kama Wajapani wakija huku na kutusukuma nyuma, ama kitu kama hicho? Hisia ile ile. Kumbukeni wao ni wanadamu.

20 Nikasema, "Hayo yote siwezi kusaidia, mimi ni Mmarekani mmoja tu, mimi ni mtu mmoja tu anayepiga kura kama tu mnavyofanya, na nina haki zile zile mlizo nazo, na kadhalika." Lakini nikasema, "Sipo hapa kuwaambia kuhusu taifa hili, nipo hapa kuwaambia juu ya Mtu ambaye atawatendea haki, huyo ni Yesu Kristo."

21 Nami nakumbuka tulipofanyiza mstari wa maombi, Mhindi kwa namna fulani ni jamaa wa kuchekesha, mwajua, kwa hiyo hakuna mtu aliyekuja kwenye mstari wa maombi. Ilikuwa kwamba ungeninii . . . ingetubidi kuwachukua na kuwasukuma nyuma kwa genge kubwa la mabawabu. Tukaitisha mstari wa maombi, hakuna mtu aliyekuja, nikamwangalia Ndugu Jack, naye akaniangalia. Hatimaye, mkalimani akarudi . . .

22 Jina lake nani yule mwanamke pale aliyekuwa na ile misheni huko nje kwenye hiyo . . . ? Ni—ninaamini yeye ni mfuasi, Assemblies of God, naam, ninasahau jina lake sasa. Lakini hata hivyo, nilikuwa kwenye vipandio vya kanisa lake . . . Ati nini? Mitchell, Bibi Mitchell. Wengi wenu ninyi watu wa Assembly of God huenda mkakumbuka. Naye . . . Tulisimama kwenye vipandio tukiwa na vipaza sauti, na ilionekana tu kama zile siku za kale za mkokoteni uliofunikwa kuwaona wameketi kote huku jua linashuka. Na maskini machifu wote, na maskini Wahindi kila mahali, nao walivukia tu mle ndani, kote kwenye kingo za mto San Carlos.

23 Ndipo basi, baada ya kitambo kidogo, mkalimani huyu, wana wakati wote wa kufanyia lolote, mwajua, kwa hiyo akarudi tu ndani, akamleta mwanamke wa Kihindi. Vema, mara alipojitokeza, vifundo vikubwa, vipana vya mikono, asingeweza kuzungumza hata neno moja la Kiingereza, akaniangalia usoni. Nikamwangalia kwa dakika chache pale, nikasema, "Huyu mwanamke ana ugonjwa wa zinaa. Si kwa sababu ati yeye ni mkosa maadili, bali jinsi imemlazimu kuishi."

Akaniangalia kwa mshangao sana, mkalimani huyo akaliweka hilo vizuri, akatikisa kichwa chake, "Hiyo ni kweli."

24 Kwa hiyo aliyefuata alikuwa ni msichana mdogo, naye aliendelea kuinamisha kichwa chake. Nikasema, "Sasa, msichana huyu mdogo," nikasema, "yeye ni wa mmoja wa watu mashuhuri katika kabila hili, naye alikuwa na homa,

ilimfanya awe kiziwi na bubu pia. Amekuwa kiziwi na bubu kwa zaidi ya miaka miwili, hakuwa amezungumza wala kusikia chochote." Nikasema, "Sasa, ninyi nyote mnamjua msichana huyu mdogo, kwa sababu yuko papa hapa kwenye hifadhi." Nikasema, "Sasa, Yesu Kristo anawapenda Wahindi, Yeye atawaponya Wahindi."

Nikamwekea mikono, nami nikawazia . . . nikasema, "Usitafsiri hili."

Na kwa hiyo, nikaomba, "Bwana, nipe kibali kwa watu hawa."

25 Basi nikamwombea huyo msichana mdogo, nami nikamwendea. Na kama umewahi kusikia lugha ya Kiapache, loo, jamani! Hmm! Kwa hiyo, nikasema, "Unanisikia?" Akageuka, akaniangalia, na maskini nywele hizo nyeusi, maskini uso huo mchafu, naye akaniangalia, nami nikasema, "Unanisikia?"

Akasema, [Ndugu Branham anaiga lugha ya Kiapache—Mh.]

Nami nikasema, "Atazungumza vizuri zaidi."

Ndipo mama yake akageuka, akasema, "Hmm! Mazungumzo yake yanakuwa mazuri sasa."

Kwa hiyo, nikasema, "Vema . . . "

26 Na mwingine, walikuwa na maskini mvulana mdogo, wakamsukuma nje ya jengo hilo dogo, maskini nywele zake zinakwaruza kama manyoya juu ya farasi, huku ameinamisha kichwa, nami nikasema, "Vema," nikamwacha huyo mvulana mdogo aniangalie, nikasema, "ana makengeza, sivyo?"

27 Naye huyo mama kwa namna fulani alikuwa mkali, akamshika tu juu ya kichwa, na kuvuta nywele zake nyuma, macho nyuma, nayo maskini macho yake yamekaa namna *hiyo*.

28 Nikasema, "Sijui kama ningeweza kupata . . . " Aliniogopa. Kwa hiyo, nilikuwa na kipande cha chingamu, nikafanya urafiki naye, nikamwacha ainuse, mwajua, akaendelea kuinamisha kichwa chake, nikamfanya ainuse, hayo maskini macho yenye makengeza yakiangalia pande zote.

29 Nikamchukua, nikamshika mikononi mwangu, nami nikawazia, "Mungu, kama uliwahi kunisaidia, na iwe sasa, ninaweza tu kupata kibali kwao, ndipo wataamini." Mnaona? Nilikuwa nimemweka kwenye maskini bega langu, maskini kichwa chake kwenye bega langu, nami nikasema, "Bwana, ninaomba ya kwamba utayanyosha macho yake."

30 Nikasema, "Sasa, inueni vichwa vyenu." Nikasema, "Sasa, kabla sijamwacha huyu mtoto aondoke mabegani mwangu, endapo macho yake hayajanyoka mimi ni nabii wa uongo; kama macho yake yamenyoka, basi aminini nimekuja na Ujumbe kutoka kwa Yesu Kristo kwa ajili yenu." Nikamgeuza

namna *hii*, basi nena kuhusu mstari wa maombi! Kulikuwa na mkanyagano. Mavumbi yakipeperuka, na kila mtu akijari-. . . Vema, tusingeweza kupata . . . Hakuna mtu angaliweza kuingia mstarini, walipigana tu, na kusukumana, na kupiga makelele, wakirukiana.

31 Na kwa hiyo, huyo, kweli aliyefuata alikuwa ni mwanamke mzee wa Kihindi, akija kutoka huko nyuma, na kulikuwa na maskini mvulana mdogo, mnene, mwenye umri wa kama miaka kumi na minane, a—alipanda tu juu ya wote, alikuwa na nguvu sana, akawa wa pili mstarini. Nami nikasema, "Mwanangu, we—wewe—wewe siwe wa pili, mwanamke huyu mkongwe ndiye anayefuata." Nisingeweza kumfanya aelewe. Naye Ndugu Jack ni mzuri sana, yeye mwenyewe mtu mdogo, mwajua, seremala, kwa hiyo akamshika tu huyo mvulana mdogo, na kumvuta akamwondoa njiani.

32 Huyu hapa maskini mwanamke huyo wa Kihindi anakuja, kamwe sisahau hilo maadamu ningali hai, magongo yake yalitengenezwa kwa fimbo mbili za ufagio pamoja na baadhi, kipande cha mbao kilichoshindiliwa juu, huku kimefungwa matambara, kukilainisha. Naye asingeweza . . . Hapana shaka ulikuwa ni ugonjwa wa yabisi kavu, naye akasukuma mbele fimbo hizi mbili, alionekana kuwa angalau na miaka themanini, basi akasukuma fimbo hizi mbili mbele, naye angepiga hatua, basi, kisha angeweka hiyo nyingine. Nilisimama tu kimya kabisa, naye akanijia, moja kwa moja, namna *hii*, huku anatetemeka, namna *hiyo*, naye akaniangalia namna *hiyo*.

33 Loo, jamani! Nikaona maskini hizo nywele zenye mvi zilizosukwa, mwajua, maskini makunyanzi hayo, yenye kilindi mashavuni mwake, na machozi yakipenya kama m—mto pale, yakishuka, yakidondoka kutoka usoni mwake namna *hiyo*, nami nikawaza, "Mama wa mtu fulani. Hapana shaka, maskini huo mkono, mnyonge pale, wenye makunyanzi, umeyapangusa machozi kutoka kwenye macho ya watoto wengi wanaolia. Shida ambazo amepitia!"

34 Alisimama tu na kuniangalia, na kamwe hakufungua kinywa chake na kusema kitu. Mara akaanza kutabasamu, akanyosha mikono, akashika mkongojo mmoja, na mmoja mwingine, akaikabidhi kwangu, kisha akaondoka pale akiwa sawa na mtu mwingine yeyote. Hakuna maombi wala chochote kile, aliamini tu. (Mnakumbuka hilo?)

35 Na yapata, nadhani ilikuwa karibu mapambazuko, nilikuwa huko usiku kucha, na kwamba [Ndugu Jack anasema, "Saa kumi."—Mh.] yapata saa kumi, saa kumi asubuhi, hiyo ilikuwa kabla ya machweo alasiri hiyo, tulikuwa tukiomba usiku huo wote, mpaka saa kumi kesho yake asubuhi, niliona Wahindi wote walioingia walikuwa wamelowa maji kufikia *hapa*, nikasema, "Wana shida gani?"

36 Naye akasema, "Vema, mwanzoni walidhani wewe ni mwongo," lakini kasema, "sasa," kasema, "kivukio kiko chini *kabisa*," lakini kasema, "walikimbilia mbugani, na kuwachukua wapendwa wao, nao wanavuka mto usiku wa manane wakiwabeba wapendwa wao kuwaleta wakaombewe."

37 Watasimama kwenye Hukumu pamoja na hiki kizazi cha wazungu, na kuwahukumu, mara nyingi baadhi ya watu hawa ambao hata hawataukaribia mlango wa nyumba ya mkutano.

38 Na kwa hiyo, ninakumbuka kisa kimoja kule, mimi... Samahani tu kwa kuchukua muda, lakini imani chanzo chake ni kusikia, tunashinda kwa neno la...la ushuhuda wetu. Na hiki kilikuwa ni kisa cha kipekee sana, kulikuwa na mzee Mhindi, walikuwa na ubao kama *huu*, nao ulikuwa na fimbo nne zikiukingama ubao huu, hawakuwa na machela ya kumbebea mzee huyo, kwa hiyo wakamwacha aweke mikono yake *hapa* juu, mwenye mvi tu awezavyo kuwa, na magoti yake yakiwa upande wa pili wa huo ubao. Na kulikuwako na jamaa wawili wakubwa waliokuwa wamembeba, wamelowa maji wawezavyo kuwa. Nikamwambia mmoja wa hao jamaa, alikuwa wa pili mstarini, nikasema, "Unazungumza Kiingereza?"

"*Kidogo*."

Nikasema, "Hivi huogopi utashikwa na nimonia?"

"La." Kasema, "Yesu Kristo amenitunza, nilimleta baba yangu."

"Hmm?" Nikasema, "Unaamini Yesu Kristo atamponya baba yako?"

"Naam, hiyo ndiyo sababu nilimleta."

Kasema, "Vema." Nikampisha, nikasema, "Mpisheni."

39 Nilimwekea tu mikono maskini jamaa huyo, nywele hizo zilizosukwa zimelala pale, huku anatetemeka namna *hii*, mwajua, nikamwekea tu mikono, nikasema, "Mungu, mrehemu, mponye kwa ajili ya Kristo."

40 Nikasema, "Mchukueni." Nikasema, "Huyo mwingine na aje." Wakapitana namna *hiyo*. Dakika chache nikasikia fujo kubwa huko nje miongoni mwa hao Wahindi, usingeweza kuona kabisa kuanzia mwisho wa taa kwa sababu ya Wahindi, nikaangalia huko nje, huyo mzee alikuwa ameubeba ubao begani mwake, akienda zake, akimpungia mkono kila mtu.

41 Mnaona? Tu—tunajaribu kulifanya gumu sana. Tunapitia moja kwa moja juu yake, tukijaribu kulipata. Mnaona? Tunajaribu kulifanya jambo fulani la kiajabu, wakati ni rahisi tu. Kadiri ulivyo rahisi, ndivyo utakavyokuwa bora zaidi. Kamwe usilirukie, kujaribu kujisukuma mwenyewe; lipokee tu, ni rahisi tu hivyo. Unaenda, unaruka juu yake, ukijaribu, hivyo ndivyo wanatheolojia wetu wanavyofanya, kuruka juu yake, ukijaribu kupata kilicho papo hapo karibu nawe. Unaona?

Rahisi sana, Biblia ilisema hata mpumbavu hapaswi kukosea. Hiyo ni kweli. Ni rahisi sana, Injili.

42 Loo, nawaambia, mimi, tutakapovuka Ng'ambo ya pili, sijui tu itakuwaje tutakapofika kule. Hapa . . . Ndege inaweza kusimama, mtu fulani kwenye uwanja wa ndege aseme, "Ndugu Branham, nilikuwa nikiumwa na *ninii* wakati . . ."

43 Hapa kwenye kituo cha garimoshi, chini, nilikuwa huko juu kabisa British Columbia, nilikuwa nimerudi mawindoni baada ya mkutano, nami nilikuwa na ndevu ndefu *hivyo*, wala sikuwa nimeoga kwa majuma manne, ni—ni—nilinuka kama farasi, nami nilikuwa tu . . . Tulikuwa na farasi ishirini na mmoja huko nyuma, na kwa hiyo ilitubidi tu kukaa na hao farasi wakati wote, nami nikatoka nje, nami nilikuwa nikivuta mifuko, maskini kofia iliyoinama chini kutokana na mvua na theluji, na masharubu yapata urefu *huo*, yakiingia mvi, na—na ma—machafu tu iwezekanavyo.

44 Ndipo tukasimama mahali padogo panapoitwa East Pine, huko nyuma kabisa British Columbia ya kaskazini kwenye Barabara Kuu ya Alcan. Nikaona baadhi ya Wahindi wakipita, wamevaa viatu vyeupe vya ngozi ya swala, na kutembea namna *hiyo*. Ndipo nikamwona maskini mwanamke mmoja, mwenye uso mwekundu akiendelea kuniangalia, sijui kama alikuwa ni Mweskimo ama Mhindi, aliendelea kuniangalia *hivi*. Nami nikaangalia tu kote, sioni jinsi alivyowahi kuuona uso wangu, ndevu zote zimetokeza nje namna *hiyo*, Nikavuta mifuko, ndipo nikahisi mtu fulani akinigusa begani. Nikageuka, akasema, "Samahani. Hivi wewe si ni Ndugu Branham?"

Nikasema, "Naam, mama." Nikasema, "Ulipataje kunijua?"

Akasema, "Ninaona picha yako."

Nikasema, "Wapi?"

Akasema, "Sleji ya mbwa hupitia hapa mara moja kwa mwaka, nayo ilileta kitabu chako kiitwacho, *Nabii Azuru Afrika*."

45 Ndugu Rasmussen, mlipata kusikia habari zake? Alipoteza ufunguo wa gari lake, nami nikaingia Dawson Creek, loo, ni jiji kubwa, yapata watu mia tano, mia sita, na moja kwa moja mwanzoni mwa Barabara ya Alcan, niliona ubao mkubwa wa ufunguo, nami nikasema, "Labda ninaweza kumfanya huyo mtu atengeneze ufunguo." Hapo alisimama mtafuta madini mzee, loo, jamani, uso wake, pua yake karibu kubwa kama ncha ya mkono wangu, imevimba, nyekundu, amevaa jaketi kubwa la manyoya, ndipo nikamwuliza mtu huyu, nikasema, "Unaweza kutengeneza ufunguo wa motokaa?"

Kasema, "La, bwana, siwezi."

Nikasema, "Asante."

46 Nikatoka nje, nikahisi mtu fulani akinigeuza, nikaangalia na ilionekana tu kama macho madogo yalikuwa nyuma ya manyoya hayo yote. Mtu huyo akaniangalia usoni, akasema, "Naam, ninaamini niko sawa."

Nikasema, "Unamaanisha nini, bwana?"

Kasema, "Wewe ni Ndugu Branham, sivyo?"

Nikasema, "Naam, bwana. Ulinijuaje?"

47 Akaanza tu kulia, machozi yakitiririka ndevuni, akanikumbatia namna hiyo. Akasema, "Mimi ni ndugu yako." Akasema, "Nina kimoja cha vitabu vyako. Nina vibanda saba ama vinane kwenye safu yangu ya mitego, inanichukua majuma mawili kuvizunguka na kwa sleji ya mbwa." Kasema, "Kwa mwanga wa mishumaa siku nyingi usiku nimepiga magoti karibu na mshumaa wa grisi huko nje katika sehemu hizo na kukuombea." Akasema, "Nilipata ubatizo wa Roho Mtakatifu," akasema, "Mimi ni ndugu yako."

Sote tutakapofika Mbinguni,
Hiyo itakuwa ni siku ya furaha jinsi gani!
Sote tutakapomwona Yesu,
Tutaimba na kupiga shangwe za ushindi.

Sivyo? Jamani, jamani!

48 Kote ulimwenguni, kila mahali, Mungu anao watoto Wake. Panda meli ya mvuke, na uanzie mahali fulani . . . Nilikuwa huko Jamai- . . . Loo, hebu nisimame tu, hiyo ni kusema, tunasimama tu, tunaendelea kushuhudia. Popote walipo, matabaka yoyote ya maisha, mahali fulani mtu fulani amesikia kuhusu nguvu za Mungu za kuwaponya wagonjwa.

49 Laiti, usiku wa leo sitaninii, sitahubiri kwa sababu ninataka kuwaombea wagonjwa usiku wa leo. Lakini kuwafanya tu mpate uzoefu sasa wa—wa mkutano kwa dakika kumi na tano zifuatazo ama kitu kama hicho, ninataka kuwakumbusha Maandiko yanayopatikana katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 14, kifungu cha 27. Nami ningetaka sasa kwamba mngekuwa tu na kicho iwezekanavyo, mnaona. Sikilizeni sasa na mshikilie maneno.

50 Ni wangapi waliopo hapa hawajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu. Loo, jamani, sote hatungeweza kufika mahali hapo kwa wakati mmoja, ni, kwa hiyo karibu nusu ya umati haujawahi kuwa mkutanoni hapo kabla. Bila shaka tunakukaribisha hapa, ndugu na dada yangu msafiri. Sisi ni raia pamoja nanyi katika Ufalme huu mkuu wa Mungu, tukifurahia uchumi Wake wa Uwepo wa Mungu na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

51 Mimi, nikiwaombea wagonjwa, sidai kuwa mponyaji, kuna Mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu, nasi tumetumwa tu kama watumishi Wake. Lakini ninatangaza ya kwamba Yesu

Kristo yuaja mara moja, ninamtazamia. Asipokuja usiku wa leo, nitakuwa nikimtazamia asubuhi; asipokuja juma hili, nitamtazamia juma lijalo; asipokuja mwaka huu, nitakuwa nikimtazamia mwaka ujao, ninataka kuwa tayari atakapokuja.

52 Nami ninaamini ya kwamba Yeye aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Nasi tunaona ya kwamba huko Sodoma ninii, kulikuwako na we—we—wenye dhambi, kundi la wenye dhambi, Wasodoma; halafu kulikuwa na kundi la Wakristo, waaminio vuguvugu ambao waliwakilisha kanisa lililoishi miongoni mwao, Lutu na watu wake, watu wa utakatifu, dhambi za mji huo ziliitesa nafsi yake yenye haki; kisha kulikuwa na kundi teule alilokuwa nalo Ibrahimu, lililoitwa litoke, na kila mmoja wao alipokea ishara. Nami ninaamini ya kwamba ishara ambayo Malaika wa Bwana alifanya, aliyedhihirishwa katika mwili pale, ilikuwa ni ishara ya dhihirisho la Kristo katika Kanisa Lake katika siku za mwisho.

53 Sasa, Yesu alisema, Yohana Mtakatifu 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Yeye pia alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu," utaratibu wa ulimwengu, "hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona," Kanisa, Waaminio, Walioitwa watoke, Wateule, "kwa kuwa Mimi," *Mimi*, si mtu mwingine bali *Mimi*, kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari." Waebrania 13:8 ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

54 Basi kama Yeye ni yule yule leo kama alivyokuwa wakati huo, Yeye ni Mwokozi yule yule, Mponyaji yule yule, Kuhani Mkuu yule yule, Bwana yule yule, Yeye ni kama tu alivyokuwa wakati huo, ila tu badala ya kuwa katika mwili wa nyama unaoitwa Yesu, Mungu anaishi katika Kanisa Lake, mwili wako, mwili wangu, ambao aliutakasa kwa Damu Yake Mwenyewe apate kutusafisha kwa kutuosha kwa maji kwa Neno, na kumtolea Mungu Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi. Kwamba Yeye, "Kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," za Kimbinguni.

55 Vema, katika Mathayo 14:27:

> Na *mara Yesu alinena akawaambia,* . . . *msiogope* . . . *Jipeni moyo*; *ni mimi; msiogope.*

56 *Msiogope, Ni Mimi.* Sasa, beba hilo niani mwako sasa, kwa uchaji, nanyi hasa mlio wagonjwa, nanyi ambao hamjaokoka, hamjaingia katika ushirika wa Roho bado, liwekeni hilo niani mwenu, nami nitaharakisha upesi niwezavyo, niitishe mstari wa maombi.

57 Angalieni mazungumzo haya, hebu na tuyaingilie, na sasa tufanye mchezo mdogo wa kuigiza kutoka kwake kusudi vijana

waweze kuyapata. Jua lilikuwa ndio kwanza litue, ama, lilikuwa linatua kwenye upeo wa macho upande wa magharibi wakati mtazamo wake wa mwisho ni kwenye Bahari ya Galilaya. Ninaweza kuona misuli migumu ya yule mvuvi mkubwa alipokuwa akisukuma maskini huo mtumbwi kwa shetri, huku gubeti yake ikisukumiwa majini, watu wamesimama ukingoni wakipunga mikono na kulia. Hatimaye alipokiondoa maskini kile chombo kwenye changarawe akakiingiza majini, akapanda mpaka katikati ya hicho chombo ambapo ndugu yake, Andrea, alikuwa ameketi kando ya kasia, na akapachukua mahali pake. Wangepiga makasia mara moja ama mbili, na kisha kuwapungia mkono watu waliokuwa ufukoni, kupiga makasia mara moja au mbili, na kuwapungia mkono watu walio ufukoni.

58 Baada ya kitambo kidogo, wakati giza lilipoanza kuingia, walikuwa hawaonekani sasa, na hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, ndiye aliyekuwa mdogo kuliko wote miongoni mwao, hapana shaka ndiye aliyengoja kidogo, akasimamisha makasia yake kwa dakika chache tu apate kupumua, kwa kuwa walikuwa na mwendo mrefu, bado, kuvuka Galilaya. Naye aliposimama apate kupumua, hapana shaka alisema kitu kama hiki, huku akipangusa jasho usoni mwake, kasema, "Ndugu, tunaweza kuwa na hakika ya kwamba Mtu tunayemfuata si wa bandia. Leo niliposimama begani Mwake, na kumwona akichukua hao samaki wadogo na kuwavunja vipande viwili, na kuangalia, mara tu Yeye alipowavunja, ikatokea sehemu nyingine ya samaki aliyepikwa. Nami nilimwona akichukua mkate huo na kuumega mkate huo, na kuwakabidhi ndugu, kila wakati alipokimega kipande cha mkate, mara tu mkono Wake ulipoondoka, kulikuwako na kipande kingine cha mkate pale."

59 Ninataka kuwaulizeni: Yeye aliachilia atomi ya aina gani? Si ngano, mkate uliookwa tayari, uliikwepa jiko, kama alivyoufanya ule mwujiza Wake wa kwanza Kanaani. Maji hayo hatimaye yangekuwa divai, yalipanda kupitia kwenye mizabibu yakaingia kwenye zabibu, zikapondwapondwa, zikawa divai. Lakini Yeye aliyakwepa hayo yote, Yeye Mwenyewe alikuwa Muumba. Kwa hiyo katika ule ufufuo mkuu, Yeye atamkwepa baba, mama, amzae huyu, Yeye atanena nasi tutatoka mavumbini, kama alivyomfanya Lazaro.

60 Na hapana shaka Yohana alisema, "Mnajua, leo imekuwa ni siku ambayo imemaliza mashaka yote niani mwangu. Haidhuru marabi na walimu wa siku hizi wanasema kiasi gani ya kwamba Yeye si Mungu, ninajua ndivyo alivyo. Kwa kuwa ninakumbuka mama yangu akinisomea Maandiko matakatifu, katika Magombo ya Kutoka, jinsi ambavyo wakati walipokuwa na njaa, kama watu hawa walivyokuwa leo hii, Mungu alishusha mkate kutoka Mbinguni, akauweka ardhini. Kwa hiyo, nilipoona. . . Nilimwambia mama, 'Mama, je, Mungu ana jiko kubwa Kule juu la kuokea mikate hiyo?' Akasema, 'La Mpenzi,

Mungu ni Muumba.'

61 "Basi nilipomwona akiumega mkate huo tena leo, nilijua Huyo alikuwa ni Muumba yeye yule. Hivi Yeye hakuonekana kama Yehova wakati aliposimama pale akiutazama huo umati, na kuumega mkate huu na kuusambaza? Nilizikumbuka hadithi za Biblia ambazo mama yangu alikuwa akinisomea kuhusu Yehova akiwalisha watu Wake chakula kutoka Mbinguni. Na leo Yehova anabaki yeye yule, maana leo hii, ndugu, tumemwona Yehova akimega mkate na kuwapa watu Wake tena na kuzidisha, hakika Yeye hana budi kuwa kile asemacho ndicho alicho, Mwana wa Mungu."

62 Basi wakati huyo kijana Yohana aliposimamishwa basi kwa muda kidogo na Simoni Petro ambaye sikuzote ilimbidi kusema kitu, naye akasema, "Vema, wakati tukipumzika kidogo, ningetaka kutoa ushuhuda wangu wa kibinafsi, kwa kuwa Yohana ametoa wake. Ninakumbuka wakati Andrea, ndugu yangu, aliyeketi hapa, alizoea kuniambia, 'Unapaswa kushuka uende ukamsikie nabii akihubiri, akitabiri ya kwamba Masihi yuaja.'

"Nami nikasema, 'Yeye huvaa nguo za aina gani?'

"Kasema, 'Alikuwa amejizungushia ngozi ya kondoo, alitoka nyikani, yeye ndiye Eliya aliyenenwa kwamba atakuja, ninaamini hilo.'

63 "Ndipo siku moja akarudi na kuniambia kuhusu Mtu mwingine kuja huku, Jamaa mdogo yapata umri wake, na yote kuhusu namna fulani ya Nuru ya ajabu juu Yake, ama kitu fulani." Kisha kasema, "Nabii huyu alisema alisikia Sauti ikisema, 'Huyu ni Mwanangu mpendwa.' Nitajuaje cha kuamini kile nabii huyo alichosema? Sijapata kumsikia, sijui lolote kumhusu, kwa hiyo nikapuuza tu jambo hilo lote kama lundo la upuuzi, nami nikafikiri ndugu yangu alikuwa ameingia wazimu.

64 "Lakini siku moja alishuka akaja kando ya bahari, nami nikawazia, 'Vema, ninaamini nitaenda kule, sijakosea sana, nitaenda nione yale Jamaa huyu anayosema.' Punde tu nilipoenda pale nilijua kulikuwa na kitu tofauti kuhusu Mtu huyo. Nami nikasema jambo moja kabla sijaenda kule, ninamkumbuka baba yangu mzee, alikuwa mzee Mfarisayo mashuhuri kama ninyi ndugu nyote mjuavyo, nami nakumbuka tulipokuwa tukivua samaki hapa baharini, yeye alikuwa mtu wa kidini sana. Nakumbuka kabla ya kutoka nje angesema, 'Simoni, maskini mwanangu, hebu na tupige magoti na kumwomba Yehova, Yeye anayemiliki samaki wote, ya kwamba atazijaza nyavu zetu usiku wa leo na samaki, kwa kuwa ninawahitaji, tunahitaji chakula nyumbani. Nami . . . tuna haja ya samaki, kwa hiyo na tuombe, Simoni.' Jinsi tulivyokuwa tukipiga magoti ukingoni na kuomba!

65 "Nilimwangalia wakati nywele zake zilipoanza kupotea, zikiingia mvi. Hatimaye, siku moja aliketi chini kando ya mtumbwi baada ya kuvua samaki wengi, kwamba Mungu alikuwa amejibu maombi, naye akasema, 'Simoni, maskini mvulana wangu, Baba anazeeka, na sina budi kujibu miito yangu, karibuni sana, huko Juu. Daima nimeomba, Simoni, ya kwamba ningeishi nipate kuiona siku Masihi atakapotokea. Sasa, Simoni, hapana shaka kutakuwako na mchafuko mwingi katika siku hiyo, kutakuwako na kila namna ya mambo yatakayoinuka kimakosa kabla tu ya huyo Masihi ajaye. Lakini nataka uwe, naamini utaiona, Simoni, kwa hiyo na—nawatakeni mwe na hakika ya jambo moja, Simoni, kamwe msilikubali isipokuwa liwe na ishara ya Masihi. Hakikisha ya kwamba ishara hiyo ya Masihi ni ya Kimaandiko. Na sasa hapa, Simoni, hivi ndivyo utakavyomjua Yeye . . .'

"Nami ninakumbuka nikiketi kwenye goti lake na kuangalia machoni mwake huku yakitetemeka na kujaa machozi. 'Baba, atakuwa na sura gani?'

66 "'Atakuwa tu ni Mtu wa kawaida, na labda hatapendwa na watu wetu. "Atakuwa ni Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko." Atakataliwa na kudharauliwa, lakini, Simoni, kutakuwako na watu wengi watakaokataliwa na kudharauliwa, lakini Mtu huyu atakuwa ni Nabii, kwa kuwa Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi."'"

67 Musa alikuwa mfano mkamilifu wa Kristo, mtoa sheria, kuhani, mkombozi, kadhalika, kama Biblia inavyosoma juu yake.

68 "Naye Musa alisema ya kwamba Mungu alimwambia ya kwamba atamwinua Nabii kama yeye, na huyu atakuwa ni zaidi ya nabii, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Nawe utamkumbuka, hata hivyo, Musa, kama vile watu wetu wote walivyomkumbuka, ama, utamkumbuka, Simoni, kama vile watu wetu wote wajuavyo manabii hutumwa kutoka kwa Mungu. Na manabii wana . . . yeye ni mfunuzi wa Neno la Kiungu, yeye ni mfasiri wa Kiungu wa Neno la Kiungu. Na kama nabii huyu akisema jambo fulani, naye Mungu aliunge mkono, basi nabii huyo ametoka kwa Mungu, kwa sababu kama akisema jambo fulani, hilo ni Neno la Mungu, ahadi ya Mungu, naye Mungu anageuka kwa nabii huyo na kuliunga mkono, na kusema ni kweli, basi mnamsikia, maana hilo ndilo agizo letu, Simoni. Usidanganyike, Simoni. Lakini sasa, Simoni, unapoona mambo hayo yakitimia, mwangalie huyu Nabii.'

69 "Basi siku hiyo yote hayo yalionekana yakinirudia upesi, kwa kuwa baba yangu amekufa kwa miaka mingi. Lakini nilipoenda kule, nikaanza kumwangalia maskini Jamaa huyo, hana uzuri hata tutamani, tulificha, tuseme, uso wetu, nikawazia, 'Hivyo ndivyo hasa Baba alivyoniambia Maandiko

yalisema kumhusu Yeye. Si tofauti na mtu mwingine yeyote, alionekana tu kama watu wengine.’

70 “Lakini nilipoenda mbele Zake, Yeye aliniangalia moja kwa moja, na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona.’ Si kwamba tu Yeye alinijua, bali alimjua maskini yule baba yangu mtauwa, aliyekuwa ameaga dunia.

71 “Nikaanguka miguuni Pake, kasema, ‘Wewe ndiwe Masihi!’” Kasema, “Hilo lilitosha kwangu, kwa kuwa ninajua baba yangu alikuwa amenifundisha Maandiko, ya kwamba hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi.”

72 Hapana shaka ilikuwa ni Filipo yapata wakati huo aliyesema, “Naam, Simoni, nilikuwa nimesimama, nikaona jambo hilo. Mnajua nilichofanya? Nilizunguka kilima kumtafuta ndugu yetu Nathanaeli, aliyeketi hapa juu. Nathanaeli, unakumbuka hilo?”

“Loo, naam, Filipo, ninakumbuka jambo hilo vizuri.”

73 “Nakumbuka nilizunguka mlima, nami ni—nikamkuta Nathanaeli akiomba chini ya mti. Ndipo nikasema, ‘Nathanaeli, njoo, umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu!’ Nawe unakumbuka uliyosema, Nathanaeli?”

74 “Ninakumbuka vema, nikasema, ‘Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti miongoni mwa hao watakatifu wanaojibingirisha?’” Ama chochote unachotaka kuliita. “‘Kungekuwa Masihi yeyote anayekuja, Yeye angekuja hapa juu kwa Kayafa kuhani mkuu, Yeye angekuja ajitambulishe Mwenyewe kwa dhehebu letu. Kwa hiyo kusingekuwako na kitu chochote kilichoinuka huko chini mle ndani ambacho, “mwana wa Yusufu” yeyote, ama kadhalika, angeweza kuwa Masihi yeyote.’ Nanyi mnakumbuka? Ninakumbuka yale uliyoniambia, pia, Filipo.”

“Ilikuwa ni nini?”

“Kasema, ‘Njoo uone.’”

75 Hilo ndilo wazo bora zaidi, usikae nyumbani na kukosoa, njoo ujionee mwenyewe. Njoo, ulichunguze kwa Neno, uone kama ni kweli. Hiyo ni theolojia nzuri. Njoo, ujionee mwenyewe.

Kasema, “Naam, ninaikumbuka.”

Kisha kasema, “Unakumbuka kile tulichozungumzia wakati tukija, Nathanaeli?” Mtumbwi ulikuwa ukiyumbayumba kwenye yale mawimbi madogo sasa, ukivuka bahari.

76 “Naam, nakumbuka.” Wote walikuwa wakitoa ushuhuda wao wa kibinafsi kumhusu Yesu, yale waliyowazia juu Yake. Na kwa hiyo, akasema, “Naam, nakumbuka vizuri. Naam nakumbuka, tulikuwa tukizungumza juu yako, Simoni, naam. Mimi. . . Akasema, ‘Unamkumbuka yule mzee mvuvi ambaye

hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe kwenye risiti kwa ajili ya samaki wako?'"

"'Naam.'"

77 "Kasema, 'Alimwambia yeye alikuwa ni nani na baba yake alikuwa ni nani. Sasa, unajua Nathanaeli, kwamba wewe ni msomi, na unajua Biblia inasema ya kwamba Masihi atakuwa ni Mungu-Nabii, tutamjua kwa ishara ya nabii.'"

"Naam, ninakumbuka hilo. Nami nakumbuka uliniambia huenda akaniambia mimi ni nani nitakapokuja mbele Zake. Loo, ninakumbuka hilo."

"Vema sasa, Nathanaeli, unataka kushuhudia kutoka hapa na kuendelea?"

"Bila shaka ninataka, ndugu. Loo, jamani!" Kama umewahi kukutana na Yesu unapenda kusimulia habari zake.

78 Ninaweza kumwona akisimama katika mashua ndogo, na kusema, "Ndugu, nilienda kule, nilishangaa ni kitu gani Mtu huyo. . .nilikuwa nimemsikia Filipo akizungumza juu Yake, nami nikawazia, 'Vema, hakika Filipo asingeniambia jambo lolote baya.' Nikafika kule, nikaona kundi dogo la watu," loo, labda kama lililo hapa usiku wa leo, ama kitu fulani, kasema, "kundi dogo la watu limesimama hapa," labda alikuwa kwenye mstari wa maombi, "basi niliposimama mbele Zake, Yeye aliniangalia, na kusema, 'Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!'

79 "Nami nikawazia, 'Sasa, ajabu hiyo, sijawahi kumwona hapo kabla, wala Yeye hajawahi kuniona hapo kabla. Kwa hiyo Yeye anajuaje kwamba mimi ni Mwisraeli? Anajuaje? Ningeweza kuwa Mwarabu, ningeweza kuwa Myunani, mbona, sote tunavalia sawa, kwa hiyo Yeye alijuaje nilikuwa Mwisraeli, wala sina hila, nilikuwa m—mtu mwenye haki, mwaminifu?' Kwa hiyo nikamwambia, 'Rabi,' sikutaka kudharau, kutomheshimu, kwa hiyo nikasema, 'Rabi, ulipataje kunijua? Hujawahi kuniona, wala Wewe hunijui, hii ndiyo mara ya kwanza tumekutana, basi ulinijuaje?'

"Akasema, 'Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.'"

80 "Naam," Filipo akasema, "Ninakumbuka yale uliyofanya, ulianguka miguuni Pake, na kusema, 'Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.'"

81 "Aisee, mnamkumbuka Rabi Lavinski kule, yale aliyosema? Alisema, 'Sasa, angalieni, enyi kusanyiko, msiamini upuuzi huo, huyo ni Beelzebuli, huyo ni ibilisi ndani ya mtu huyo, akifanya hivyo, yeye ni mpiga ramli. Mnaona? Mnakumbuka yale Yesu aliyomwambia? Alisema, 'Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja, Naye atafanya jambo lile lile, basi ukisema neno dhidi Yake, hutasamehewa kamwe katika

ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.' Mnakumbuka hilo?"

"Naam, naam, kumbuka hilo."

Hapana shaka ilikuwa ni Andrea, aliyeketi karibu na Petro, basi, aliyesema, "Je, naweza kushuhudia, ndugu zangu?"

"Naam."

82 Kasema, "Ninataka kuzungumza kwa niaba ya kundi letu lote." Kasema, "Wakati, siku hiyo, tulipokuwa tukishuka kwenda Yeriko kutoka Yerusalemu, tukishuka kwenda Yeriko, tulishuka moja kwa moja mlimani, bali alikuwa na haja ya kupitia Samaria, daima tulishangaa. Sasa, ninakumbuka Yeye akiwaambia hao makuhani siku hiyo, kwamba Yeye alisema, 'Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.' Kwa hiyo, tulimwona siku hiyo akipitia kwenye umati wa viwete, vipofu, vilema, waliopinda, waliopooza, kisha akamwona mtu amelala kwenye godoro, kasema, 'Jitwike godoro lako uende nyumbani mwako.' Mtu huyo akamtii.

83 "Kuhani akamhoji, Naye akasema, 'Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe.' Naye alijua huyo mtu alikuwa katika hali hiyo. Ndugu, hilo lilitosha, ya kwamba Yeye alikuwa . . . Alijua, Mungu alikuwa amemwonyesha la kufanya, akamwonyesha ni nani, mahali mtu huyo alipokuwa, alijua alikuwa hivyo kwa muda wa miaka thelathini na minane, hakuwa amepooza, ama hakuwa kiwete, angeweza kutembea, kasema, 'Ninaposhuka, mtu fulani ananitangulia.'"

"Naam, ninakumbuka hilo."

84 "Na, kwa namna fulani, Yeye aliongozwa kiajabu; nasi sote tunajua hilo. Tukaenda mpaka Samaria. Na si ni ajabu? Tulipofika tu nje ya mji pale kwenye kisima kile, Yeye aliketi kwenye kisima hiki, na kututuma sisi sote."

"Naam," ndugu wakasema, "Naam, mimi . . . mbona, tunakumbuka hilo, Andrea, vizuri sana."

85 Kisha kasema, "Tuliposhuka kwenda mjini, Yohana, huko ndiko ulikojitokeza na kutaka kuuteketeza huo mji, wajua, lakini, maana walitunyima chakula. Lakini tukarudi, na unajua tuliporudi kupitia vichakani kule, tulishangaa sana tulipomwona Bwana wetu akizungumza na mwanamke, msichana mdogo, mwanamke mdogo, labda wa umri Wake. Nanyi mnakumbuka, alikuwa tu akivuta mtungi wa maji tulipokuja, kwa hiyo, tulitaka kuona kile Yeye angefanya. Kwa hiyo, Yeye akasema, 'Mwanamke, nipe maji ninywe.'

86 "Na upesi akamwangalia, na kusema, 'Si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria mambo kama hayo, hatuna uhusiano wowote, tuna ubaguzi hapa, hupaswi kuniambia jambo kama hilo.'

87 “Naye akasema, ‘Lakini kama ungejua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, nami ningekupa Maji ambayo huji hapa kuchota.’

“‘Mbona,’ akasema, ‘Kisima ni kirefu, huna kitu cha kuchotea.’

“Mnakumbuka, ndugu, jinsi sisi sote tulivyojipenyeza chini ya kile kichaka na kusikiliza tuone kile Yeye angesema?”

“Naam, ninakumbuka jambo hilo, moja kwa moja nyuma ya kisima pale.”

88 “Pia, Andrea, unakumbuka, nilijaribu kukisukuma kichwa chako chini, ukijaribu kuchungulia ukutani? Na kwa hiyo, tulikuwa tukisikiliza tuone kile Yeye angemwambia mwanamke huyu. Kwa hiyo, akamkaribia zaidi, naye akasema, ‘Baba zetu waliabudu katika mlima huu, Wewe wasema huko Yerusalemu.’

89 “Unakumbuka mazungumzo yaliendelea kitambo kidogo? Na baada ya kitambo kidogo, akamtazama moja kwa moja usoni, kisha akasema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’

“Mnakumbuka alivyosema? ‘Sina mume.’

90 “‘Loo,’ tuliwazia, ‘sasa, sasa kitu fulani kilimshika, sasa Yeye amekipata! Mwanamke huyo akasema . . .’ Sasa, tunajua kama angesema uongo, Naye angekuwa Mungu wetu, Bwana wetu, tunajua ya kwamba mwanamke huyo labda angekufa, papo hapo alipo.” Hiyo ni kweli. Ati kukanusha Neno la Mungu moja kwa moja mbele Zake? “Kwa hiyo tukashangaa ingekuwaje. Akasema, ‘Sina mume.’

91 “Akasema, ‘Ulisema kweli.’ Kwa hiyo tulishangaa itakuwaje, ndipo tunamsikia akiinuka tena, kasema, ‘Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako, kwa hiyo ulisema kweli.’

“Mnakumbuka sura ya mwanamke yule? Nywele zake zikaanguka chini, macho yake makubwa, mazuri yakaangalia huko nje, akajikuna kichwani, akasema, ‘Bwana . . .’

“Sasa, Yohana, tulia, ninajua uliyosema, ‘Atasema Yeye ni Beelzebuli.’” Mnaona?

“Lakini akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.’”

92 Alijua zaidi juu ya Mungu kuliko wahubiri wajuavyo, alisema . . . katika hali hiyo. Loo, naam, ujuzi wa kitheolojia uliofunzwa kupita kiasi unakuondoa Kwake, wakati mwingine, mbali zaidi ya kutembea mtaani.

93 “Sasa, hapo kasema, ‘Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sisi Wasamaria tunajua ya kwamba yuaja Masihi, ambaye anaitwa Kristo, Mtiwa Mafuta, yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake, nasi tunajua atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya, kwa sababu hiyo itakuwa ni ishara ya Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii aliyetumwa na Mungu. Tunajua ya kwamba Yeye yuaja.’

"Yesu alisema, 'Mimi Ndiye.'" Loo, jamani! "'Mimi ninayesema nawe Ndiye.'

94 "Ndipo akaangalia tena, akaangusha mtungi huo wa maji, akakimbia mjini mbio alivyoweza. Mnakumbuka tu—tulienda kule, tukasema, 'Kula Mwalimu, kula Mwalimu'?

"Akasema, 'Nina chakula msichokijua ninyi.'

95 "Nasi tukashuka kwenda mjini, nao hawa hapa watu wakitoka. Nasi tunamkumbuka mwanamke huyo akishuka kwenda barabarani, tungeweza kuisikia moja kwa moja kutoka pale kisimani, watu wote sokoni, alikuwa akisema, 'Njoni, mwone Mtu! Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hii si ndiyo ishara ya Masihi? Naam, njoni mwone Mtu aliyeniambia yale niliyofanya. Huyu si Ndiye Masihi?'

96 "Na ndugu, mnakumbuka wakati watu hao wote walipokuja huko nje, nao wakaamini ushuhuda wa mwanamke huyo, na kumkubali kama Masihi. Loo, sote tulishuhudia jambo hilo, kwa hiyo sote tunajua," hapana shaka walisema, "ndugu, kwamba *tunajua* ya kwamba Yeye ndiye Masihi.

97 "Naye anatuahidi sasa tusiwaendee Mataifa yoyote, hao watakuwa kwa ajili ya wakati mwingine, bali nendeni, hasa, kwa kondoo waliopotea wa Israeli. Mnaona? Sasa, ajabu Yeye amejitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi, amejitambulisha Mwenyewe kwa Wasamaria, bali si kwa Mataifa. Labda atafanya hivyo baadaye, hawamtazamii Masihi."

98 Sasa, hapana shaka ilikuwa yapata wakati huo ambapo Shetani aliangalia juu ya kilima baada ya kuingia giza. Shetani anaogopa nuru, ibilisi yeyote anaogopa nuru. Hiyo ni kweli. Kitu chochote kiovu kitambaacho, kinaogopa nuru.

99 Hebu mchukue mnyama mwitu katika misitu ya Afrika, ama uwe huko nje ukiwinda, mulika tu nuru, hao wanatoroka, wanaogopa nuru. Mchukue maskini kombamwiko mbaya, tupa kiini cha tofaa chini mahali fulani, kukiwa na giza atakuja karibu akinyofoa, washa tu taa na umwangalie akikimbilia mafichoni, bila shaka. Buibui, na kadhalika, watatoroka, wanaogopa nuru. Hiyo ndiyo sababu watu wanaogopa mikutano hii ya kale, ya Roho Mtakatifu. Watoto wa giza hufanya kazi gizani, watoto wa Nuru hutembea Nuruni. "Ninyi ni Nuru ya ulimwengu, mji ulio juu ya mlima." Msiweke pishi juu Yake sasa. Mnaona?

100 Shetani aliangalia mara giza lilipoingia, akasema, "Vema, nadhani wakati umewadia kwangu kuanza kuzurura kwenye vilabu vyote vya usiku, na muziki wa makelele, kila kitu." Kasema, "Sijui hao wanafunzi na—na Yesu wako wapi." Kwa hiyo wakaangalia, na wakati yeye na pepo wake wote walipotazama, hao hapo baharini bila Yeye. Kasema, "Sasa

ni nafasi yetu! Wameenda bila yeye, sasa tunaweza kujilipizia kisasi."

101 Hilo ndilo tu analotazamia mimi na wewe, kuondoka bila Yesu wakati mmoja. Ninasema hili kwa uchaji na heshima: ninahofia hivyo ndivyo Wapentekoste wanavyofanya. Mnayaendea majengo makubwa, na madhehebu makubwa, na mashirika, nanyi mmemwacha. Mna shughuli nyingi sana katika miradi ya ujenzi, mlisahau ile misheni ndogo huko chini mtaani, na tari la kale, lile gita; mnaogopa hukumu za jela, na kadhalika tena, mnaona. Kuna kasoro, mliondoka bila Yeye, mkaingilia shamrashamra, mipango, na kadhalika, na kumsahau Yeye. Hiyo ndiyo sababu dada zetu hukata nywele zao, na kuvaa maskini nguo hizi chafu, na mashemasi wanawekwa kanisani . . .

102 Ninajua kanisa la Holiness, kanisa kuu la Kipentekoste, moja ya makanisa makubwa sana Marekani, nami najua rafiki yangu kwenye hiyo . . . mwanamume mmoja akihudhuria kanisa hili alikutana na mwanamke, msichana mdogo mle ndani aliyempenda kuliko alivyompenda mke wake, naye alikuwa na msichana mdogo mzuri, ndipo akamwacha mkewe, akamwoa msichana huyu wa kanisa, nao wakamfanya shemasi baada ya hapo. Ndugu, naam, alienda kombo bila Yeye, hilo tu ndilo nijualo, ndugu. Naam. Kwa sababu alitoa sadaka kubwa.

103 Watu wameanza kuangalia sana mambo ya pesa, na mavazi, na mambo mazuri, afadhali uangalie *juu*, afadhali muuondokee upuuzi huo, maana, kumbuka, huo ndio mwelekeo wa Laodikia, ambao wakati wa kanisa utaingilia. Humchefua Mungu tumboni Mwake, anawatapika tu kutoka kinywani mwake, Yeye alisema. Kutenda tu kama Wakristo, anataka Wakristo halisi, waliozaliwa mara ya pili wenye imani halisi, ya kweli kuamini kila Neno analoandika Mungu. Sasa, sitaki kuanza mambo hayo kwa sababu mimi huwaweka hapa muda mrefu kupita kiasi.

104 Sasa angalieni, ndipo Shetani akawaona huko nje bila Yeye, akasema, "Hii hapa nafasi yetu ya kujilipizia kisasi sasa."

105 Na hivyo ndivyo amefanya na kanisa. Niliitwa leo na baadhi ya wadhamini wangu kwenye mkutano, waliniita mwendo mrefu alasiri ya leo, kundi la wahudumu wa Kipentekoste, si Baptisti, Presbiteri, wahudumu wa Kipentekoste, nao wakakiri kwamba hawakuwa wameamini katika uponyaji wa Kiungu, na hawakunitaka humo mjini, wala wasingeudhamini mkutano ambapo waliwaombea wagonjwa. Wahudumu wa Kipentekoste! Inasikitisha, sivyo?

106 Nilipata simu nyingine, kasema, kutoka kwa kundi lililosema, "Ukiacha kundi lingine likae jukwaani pamoja nawe, hatutakuwa na uhusiano wowote nalo."

107 Hiyo ni mbaya zaidi kuliko hapo awali. Kuna nini? Waliondoka bila Yeye. Upendo wa Mungu moyoni mwetu

unatulazimisha kufikia kila dhehebu, kila mahali. Inapofikia mahali ambapo huwezi kuwa na upendo wa kumhurumia kila mwanadamu, jambo fulani limekupata. Mungu alikupenda sana wakati ulipokuwa mwenye dhambi, mgeni, mbali na Mungu, adui wa jumuiya ya Mungu, Yeye alikupenda sana hata akayatoa maisha Yake kwa ajili yako, hakika.

108 Unapata roho ndani yako, wewe ni bora kuliko mtu mwingine, basi—basi wewe ni mbaya kuliko mtu mwingine yeyote nimjuaye. Sijali kama wewe ni sahihi sana katika theolojia yako, nia na malengo yako si sahihi. Afadhali niwe—afadhali nikosee katika the—theolojia yangu, kuliko kukosea moyoni mwangu. Hiyo ni kweli. Roho wa Mungu anakaa moyoni mwako.

109 Katika bustani ya Edeni mtu alichukua ninii ya—yake . . . alipatana. Sasa, katika bustani ya Edeni kulikuwa na chaguo lililofanywa na mwanadamu: Ibilisi alichukua kichwa chake, Mungu akauchukua moyo wake. Kisha anamtuma kwenye seminari, anamgandamiza kwa theolojia nzuri, na kumkaushia mle ndani, ndipo anarudi nje, kichwa chake kimejaa majivuno, kikubwa mno hakiwezi kuvaa kofia ya kawaida. Kisha atoke akiwa na uchungu moyoni mwake dhidi ya raia mwenzake wa Ufalme? Huyo si Mungu. Sawa.

110 Shetani aliwaona wakienda namna hiyo, bila Mungu, na kwa hiyo akasema, "Sasa hebu na tuwaangamize."

111 Na hiyo ndiyo njia nzuri tu ya kuiangamiza, pia. Ndugu, unapofikia mahali ambapo huwezi kunyosha mkono uani, uvuke barabara, na kushirikiana, na kumwita mtu ndugu, kwa sababu tu huenda kukawa na tofauti ndogo mno (Unajuaje wewe si tofauti kidogo machoni pa Mungu, kitu fulani kidogo.), na uwe ndugu? Mbona, bila shaka! Ndugu, mahali pako ni madhabahuni, sawa kabisa, jipatanishe na Mungu. Nisingetaka huyo pepo mchafu awe juu yangu. Hiyo ni kweli. Ninasikitika kuona hayo yakinyemelea katika makundi ya Kipentekoste, pande zote zake, pia, yanatoka pande zote. Mmoja, chungu hakiwezi kuiita birika kuwa ni nyeusi, kwa sababu ni sita tu ya moja, nusu dazani ya nyingine, kwa hiyo wako pande zote mbili.

112 Lakini, loo ndugu, kamwe usiruhusu jambo hilo ovu liwapate ninyi wanaume. La, bwana, ndugu. Shikamaneni kama sukari ya rojorojo kwenye asubuhi yenye baridi, kabisa kabisa, shikamaneni pamoja kabisa, mshikamane. Hiyo ni kweli. Kwa . . . Naam.

> Kibarikiwe kifungo kifungacho
> Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
> Ushirika wa watu wenye nia moja
> Ni kama ule wa huko Juu.
>
> Mbele ya kiti cha enzi cha Baba yetu,

Tunamwaga maombi yetu ya pamoja; (Hiyo ni kweli.)
Hofu zetu, matumaini yetu, malengo yetu ni mamoja,
Faraja zetu na mahangaiko yetu.

113 Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa, naam, bila shaka, sio wachoyo, wenye ubinafsi, wasiojali, waovu. Matunda ya Roho ni upendo, furaha, uvumilivu, upole, utu wema, imani, subira. Jambo ndilo hilo, hilo ndilo tunda la Roho.

114 Mwajua mti, kama mti una maganda ya mkuyu na matofaa yanakulia juu yake, ni kitu gani? Ni mtofaa, uhai ulio ndani ya huo mti huzaa matofaa. Haidhuru theolojia yako ni nini, sahihi au si sahihi, kama unazaa tunda baya, wewe ni mti mbaya, ndugu. Yesu alisema, "Kwa tunda lao mtawatambua," si kwa mti wao, bali kwa tunda lao. Hiyo ni kweli. Kweli.

115 Sasa, aliwaona bila Yesu. Ndipo akaanza kuwapulizia pumzi yake ya sumu, ndipo dhoruba kubwa ikashuka, na ile meli ndogo ilikuwa karibu kuinama, huku na huko, juu na chini, huku na huku. Maskini mtumbwi huo ulijaa maji, nguzo ya mlingoti ikalipuliwa, makasia yakavunjika. Hiyo ni kama hali ya ulemavu tunayoingia. Hiyo ni kweli—hiyo ni kweli.

116 Akaanza kupuliza pumzi yake, akisema, "*Whiu!* Wewe ni mfuasi wa dhehebu letu, la sivyo wewe si mfuasi wa chochote. Sisi ndio tulio sahihi, hao wengine wamekosea. Jitenge." Loo, jamani! "Naam, siku za miujiza zimepita. Aa, huo uponyaji wa Kiungu, hakuna kitu kwake. Uh, hakuna kitu kama *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*." Loo, jamani! Mnaona, hizo ni pumzi za sumu za Shetani, "Usiwe na uhusiano wowote naye, yeye haamini kama tunavyoamini sisi."

117 Kuna imani moja tu, hiyo ni imani ya Mungu. Hiyo ni kweli. Imani ya Mungu, imani yako ya kibinadamu haiendi mbali sana, bali imani ya Mungu ndani yako:

Inakufanya umpende kila mtu,
Inanifanya nimpende kila mtu.

118 Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo imani ya Mungu inavyokufanyia, inakufanya uwe na hisia ile ile aliyokuwa nayo Yesu, kwa sababu Roho wa Kristo yuko ndani yako.

119 Matumaini yote yalikuwa yamekwisha, walikuwa karibu tu kuzama. Loo, walikuwa karibu kushikana, na kusema, "Kwa nini tuliondoka bila Yeye? Kwa nini hatukumshurutisha aende pamoja nasi?"

120 Lakini mnajua nini? Yeye hufanya mambo kama hayo wakati mwingine, aone tu kile tutakachofanya. Nafikiri Yeye alifanya hivyo wakati huo. Badala ya kuwaacha wote pamoja, mnajua alilofanya? Alijua hilo lingetukia. Anajua jambo hili sasa hivi, linaloendelea sasa lilikuwa linaenda kutukia. Lakini mnajua

alilofanya? Alipanda kilima kirefu kuliko vyote vilivyokuwako Palestina, alipanda juu ya kilima kusudi aweze kuona kote kote baharini apate kuwatazama. Loo!

121 Alipokufa pale Kalvari, alipanda ngome za Kalvari mpaka akaendelea kupanda kwenye ile asubuhi ya Pasaka, mpaka akapanda kupita mwezi, nyota, jua, mpaka angeweza kuona kutoka Umilele kuingia Umilele. Jicho Lake liko kwenye shorewanda, nami ninajua Yeye anauangalia mkutano huu usiku wa leo. Anataka kuona kile tutakachofanya.

122 Matumaini yote yalikuwa yamekwisha, walidhani kila kitu kilikuwa kimepita, walikuwa karibu kuzama. Basi wakati ule muhimu sana, wakati alipokuwa amewaangalia, na Huyu hapa anawajia akitembea juu ya bahari iliyochafuka. Na sasa, kosa la kuhuzunisha walilofanya, ninataka kusema katika kufunga, ndilo kosa lile lile la kuhuzunisha ambalo kanisa linafanya siku hizi, walimwogopa. Walidhani Yeye alikuwa ni mzuka, kivuli, mzuka fulani, kupiga ramli, na pepo, hivyo ndivyo walivyowazia, wakaanza kutetemeka.

123 Lakini sikiliza Neno hilo la kufariji: “Msiogope; jipeni moyo; ni Mimi.”

124 “Ni Mimi!” Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, Msaada pekee ambao wangeupata, nao waliuogopa.

125 Na leo hii, kitu pekee kitakachovunja vizuizi, kitu pekee kinachoweza kutuunganisha pamoja kama ndugu na Wakristo, kitu pekee kinachoweza kutuleta pamoja tena ni Roho wa Mungu, ama, upendo wa Mungu, ambao umemwagwa ndani ya mioyo yetu, ujumbe wa neema kutoka kwa Mungu kwamba hatujagawanyika, sisi sote ni Mwili mmoja. Mungu huwaponya jinsi tu walivyokuwa . . . hata wawe nini; hatujagawanyika.

126 Wanamwona Roho wa Mungu aliyeahidiwa na Kristo Mwenyewe. Katika siku za mwisho Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika Sodoma,” wakati Malaika yule aliyetumwa na Roho wa Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili, akila nyama ya ndama, akinywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, kunywa mtindi, maziwa matamu, chochote kilichokuwa, akila siagi na ugali wa mahindi, ameketi pale akila kama mwanadamu, alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, Mgeni, kamwe hakuwa amewahi kuwa huko hapo kabla, Ibrahimu hakuwa amewahi kumwona. Kadiri Ibrahimu alivyojua, Yeye hakuwa amemwona kamwe. Naye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

127 Loo! Alijuaje alikuwa ameoa? Alijuaje alikuwa na mke? Pia alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

128 Ningewazia Ibrahimu alisema, “*Mwongozo wangu ulikuwa sahihi*!” Kasema, “Yuko hemani nyuma yako.”

129 Kasema, "Ibrahimu, nitaitimiza ahadi Yangu kwako." Angalia, si Malaika, si mwanadamu, bali "*Mimi*, nitatimiza ninii *Yangu*," (Ni ahadi ya jinsi gani!) "kile *Mimi* nilichokuahidi."

130 Loo, jamani! Hivi hamwezi kuona ilikuwa ni Mungu? Ibrahimu alisema ilikuwa ni Mungu, yeye alimwita Elohimu, Bwana Mungu, Muumba. *El, Elah, Elohimu* maana yake ni "Anayejitosheleza kwa yote na Anayeishi Peke Yake." Amina. Yeye alikuwa Anayeishi Peke Yake, Elohimu, aliyedhihirishwa katika mwili wa nyama, akila na kunywa kama mwanadamu, ambaye alijua alikuwa Ibrahimu.

131 Mungu yeye yule aliyedhihirishwa, na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona. Nilikuona ulipokuwa chini ya mti." El, Elah, Elohimu. Mnaliona?

132 Na katika siku za mwisho, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Usimwogope Mungu, Ndiye kitu pekee kinachoweza kukusaidia.

"Atatusaidia sisi Wamethodisti?"

Naam.

"Atusaidie sisi Wabaptisti?"

Naam.

"Atusaidie sisi wa Umoja?"

Naam.

"Uwili?"

Naam.

"Utatu?"

Naam.

"Unne? Utano?"

133 Sijali wewe ni nani, ni msaada kwa ajili yenu nyote, msiogope jambo Hilo. Ujumbe wa Biblia ya Mungu kwa kila mmoja wenu: "Yeyote atakaye, na aje anywe kutoka kwenye chemchemi ya Maji ya Uzima bure."

134 "Usiogope; ni mimi," alisema Yesu. "Na *Mimi* nitakuwa pamoja nanyi," *Mimi*, hicho kiwakilishi tena, kiwakilishi nafsi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Amina. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

135 Wakati alipokuwa, jana katika siku Zake alikuwa ni Nguzo ya Moto. Alidhihirishwa katika mwili, kasema, "Nalitoka kwa Mungu, tena naenda kwa Mungu."

136 Siku chache baadaye, baada ya kufufuka Kwake, Sauli, akitoa vitisho vikali, alishuka kwenda Dameski, Nuru, Nguzo ya Moto ilimwangusha chini, akasema, "U nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

Petro alikuwa gerezani, ile Nguzo ya Moto ikaingia dirishani. Petro akawaza, "Ninaota ndoto sasa."

137 Akasema, "Njoo, unifuate Mimi." Malango yalifunguka yenyewe, akapita moja kwa moja karibu na walinzi, hakutambua ilikuwa ni Mungu mpaka alipokuwa nje. Amina. Ninampenda, nanyi je?

138 Hebu, sasa wakati wangu umepita kwa dakika tano, hebu tumwimbie tu wimbo huu mdogo, ninyi watu wote, kila mtu. "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza."

139 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya Neno Lako, Neno Lako ni kweli. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alidhihirishwa mbele zetu katika mwili." Katika Kitabu cha Waebrania ilisema, "Neno la Mungu," Kristo, bila shaka, "lina nguvu na ni kali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, likichoma hata kugawanya mifupa na mafuta yaliyomo ndani yake, tena ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo." Ee Mungu, uturehemu! Tujalie, Baba.

140 Jitambulishe Mwenyewe usiku wa leo katika mwili wa kibinadamu kwa kufanya mambo yale yale uliyofanya huko nyuma, wapate kujua, na tutakaposimama kwenye Kiti cha Hukumu hakutakuwa na udhuru. Baba, chukua dawa Yako ya macho ya Roho usiku wa leo, na uyafungue macho ya watu, wapate kuona ya kwamba ni Wewe, ya kwamba ni Roho Wako, Wewe hujafa, Wewe u hai milele. Jalia wengi wa watu, hata kwenye. . .kama yule mwanamke alivyoligusa vazi Lake, jalia waponywe kwa neema, kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wangu. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]
> . . .mtini Kalvari.

141 Sasa kwa utamu sana. Unampenda, kweli unampenda? Inakufanya umpende kila mtu, sivyo? Vema sasa, tunapomwimbia tena kwa upole na utamu, kila mtu na apeane mikono na mtu fulani tu, kwa utulivu, moja kwa moja karibu nasi.

> Mimi. . .
> Kwani Yeye kwanza. . .
> . . .kununua wokovu wangu
> . . .mtini Kalvari.

142 Sasa hebu na tuabudu tu huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa utulivu. Aisee, uvumisheni sasa. Wazia tu jinsi alivyo mwema kwako. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ee Mungu!

143 Wazia tu moyoni mwako sasa, weka mkono wako pale Kalvari, "Ee Mwana-kondoo unayekufa, Damu Yako ya thamani kamwe haitapoteza nguvu zake." [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Wasemaje? Ati nini? Loo, labda, naam, labda ninaweza.)

Kwa nini unampenda? Hebu wazia tu, kwa nini unampenda?

Kwani Yeye kwanza . . .
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

144 Baba, tunakushukuru sasa kwa ajili ya ushirika huu mzuri. Loo, jinsi tunavyoupenda, Bwana! Ogeni tu kwenye ile Chemchemi, tukijiosha wenyewe katika uzuri wa haki Yake, na utakatifu, na nguvu Zake. Dhambi zetu zote zimetoweka, Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na hiyo. Tunajiandaa kuingia kwenye Kiti cha Enzi sasa, Bwana, kuomba fadhili.

145 Una kundi la watoto wagonjwa hapa, Baba, wamekuja, usiku wa leo, kwa sababu wanakuamini Wewe. Nami nimekuja kuwaletea Ujumbe. Ee Mungu, baadhi ya watu hawa humu ndani watakufa mara moja usipowasaidia. Madaktari wetu wapendwa wa humu duniani wamewakatia tamaa baadhi yao, bila shaka. Baadhi yao ni vilema, na vipofu, na kitu ambacho madaktari hawajui la kufanya juu yake. Baba, Wewe ndiwe Muumba.

146 Daudi, wakati mmoja, kama tulivyonukuu, alikuwa akiwachunga kondoo wa baba yake, Mungu, jalia nichukue tu mahali pake usiku wa leo, niwachunge kondoo wa Baba. Siku moja simba, adui aliingia, akamnyakua mmoja wa hao kondoo, na kukimbia, mwana-kondoo, wala hakuwa na kitu ila, kombeo dogo tu, bali alimfuatilia huyo simba, alikutumaini Wewe, akamwua huyo simba, akamrudisha huyo mwana-kondoo.

147 Baba, kuna wengi wao hapa usiku wa leo wagonjwa na wanaoteseka ambapo sayansi ya tiba imeduwazwa, hawajui la kufanya. Wamekuja hapa usiku wa leo, wao ni kondoo Wako, ninachukua kombeo hili dogo la maombi, nami ninawafuatilia, Bwana. Tupe nguvu za imani kumwua simba huyo, ibilisi huyo, kansa hiyo, huyo ibilisi ambaye amewalemaza, ama chochote kile, tupate kuwarudisha kwenye zizi la kondoo kwa ajili Yako, kwa kuwa Baba yetu hataki kuwapoteza kondoo Wake.

148 Tusamehe kutokuamini kwetu, Bwana, na uziwashe moto nafsi zetu kwa Roho Wako. Tunatambua ya kwamba uponyaji tayari umenunuliwa kwa ajili yetu, kwa kuwa "*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi," wakati uliopita, "*tuliponywa*."

149 Sasa, tujalie, Bwana, kwamba Wewe utakuja usiku wa leo katika mkutano huu, na utafanya jambo ulilofanya kama tu

ulivyofanya ulipokuwa hapa duniani, maana Wewe uliahidi itatendeka katika siku hii.

150 Na tutakapoondoka mkutanoni usiku wa leo, jalia tujisikie kama Kleopa na hao wengine wakitoka Emau, wakati ulipofanya jambo fulani pale kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, walijua huyo alikuwa ni Yesu yeye yule, alikuwa amefufuka na alikuwa akifanya tu kama alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Kwa uchangamfu walikimbia na kumwambia kila mtu, "Hakika Bwana amefufuka katika wafu!" Nao wakasema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi?"

151 Ninaomba, Baba, ya kwamba hawataogopa, usiku wa leo, wakati Wewe umekuwa ukizungumza nao katika roho yao. Au jalia watambue ya kwamba ile Sauti ndogo tulivu iliyovutia usikivu wa nabii, ule upepo wenye nguvu ukienda kasi uliopiga juu ya pango, haukumwamsha nabii sana, ngurumo na radi, damu na mafuta, na kadhalika, yote yalimwagwa chini, bali hayakumvutia nabii, lakini wakati hiyo Sauti ndogo tulivu iliponena, ndipo nabii alipoufunika uso wake na kutoka, Mungu alinena naye.

152 Mungu, hebu na tuutie uso wetu utaji usiku wa leo, na tutoke nje, tusikie kutoka Kwako. Jalia tusiogope, jalia tujifunike kwa Neno la Mungu, tutembee juu ya ahadi Yake sasa, ile Sauti ndogo tulivu ya ahadi kwa Neno, na kukuona ukitenda mambo haya tunayoomba usiku wa leo. Tunayakabidhi yote Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ninataka kuombea jambo hili sasa hivi.

153 Bwana Yesu, Wewe uliahidi jambo hilo. Siku moja, imeandikwa na mwandishi, ya kwamba wana wa Israeli walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, nayo Bahari ya Shamu ikawazuia, mojo kwa moja kwenye wajibu wao, Bahari ya Shamu ilikuwa ikiwazuia wasiingie kwenye nchi ya ahadi, naye mwandishi alisema ya kwamba Mungu aliangalia chini kupitia kwenye ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, ndipo Bahari ya Shamu ikaogopa, ikafingirika nyuma, nao wana wa Israeli wakaenda zao kwenye nchi ya ahadi.

154 Sasa, Baba, ahadi ni kwamba ungetuponya, ya kwamba umetuponya, na mashaka yako njiani, ushirikina, matatizo ya kila namna, sasa naomba Mungu asiangalie tu kupitia Nguzo ya Moto usiku wa leo, bali kupitia Damu ya Mwanawe Mwenyewe.

155 Jalia hao pepo wanaowashikilia watu walio wagonjwa waliotuma leso hizi humu, wakati leso hizi za ishara zitakapowekwa juu ya hao watu, jalia ibilisi huyo awaachilie, nao waende kwenye nchi hiyo ya ahadi ya afya njema.

156 Tujalie, Bwana, liko kwenye wajibu. Tunatuma leso hizi, katika Jina la Yesu, kwa kusudi hilo, jalia zirudishwe kwenye ahadi ambayo Mungu aliwapa, na hiyo ahadi: "Zaidi ya mambo

yote, nataka, naomba mfanikiwe katika afya," ili waweze kumtumikia Mungu. Amina.

Wale wanaozimiliki wanaweza kuzichukua baada ya ibada.

157 Sijui jinsi tutakavyofanyiza mstari wa maombi hapa juu, mstari, kuta zimejaa. Ninyi nyote mlisambaza kadi ngapi za maombi? Hamsini? Zilikuwa zipi? Za A, za B, ama...? Za C? Hebu tuone kile tunachoweza kufanya. Kuna nafasi kwa mstari kati yenu nyote na huo ukuta hapo, ndugu? Je, mstari ungeweza...? Hamngejali hilo? Hilo ni sawa. La, msininii, msiondoke njiani mwenu, tutafanya...tunawatakeni msimame papa hapa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

158 ...tofauti kama nikiwaombea au la, hilo halina uhusiano sana nalo, si mikono yangu, ni mikono Yake. Mnaona? Mnaona? Hiyo ndiyo sababu nina nyakati hizo...Sasa, kumbukeni, kama kulikuwa na jambo lolote ulimwenguni ningeweza kufanya kuwasaidia, ningelifanya. Lakini hakuna kitu ningaliweza kufanya kuwaponya, ila kuwapa tu ujumbe ya kwamba Kristo tayari amewaponya. Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? Mnaona? Mnaona? Yeye...Ni wangapi wanaojua ya kwamba kila dhambi ulimwenguni ilisamehewa wakati Yesu Kristo alipokufa msalabani? Vema. Basi unafanya nini unaposikia Neno? Unalikubali. Hiyo ni kweli. Na halafu kama unaliamini wewe ni...umeokoka.

159 Basi ni wangapi wanaojua wakati Yesu alipokufa msalabani ya kwamba kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa? Yeye alimponya kila mgonjwa. Bila shaka. Basi mtu yeyote angefanya nini? Kama tayari umetolewa kwenye duka la rehani, kama jamaa fulani amesimama pale akiwa na risiti ya ukombozi, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuupokea. Unaona? Hiyo ni kuuchukua tu, uko huru, si lazima...[Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Wasemaje? Niliita hadi ishirini na tano. Nimewaingiza wote ndani, sawa.)

160 Sasa, sasa, katika mstari huu wa maombi, jambo pekee nitakalofanya ni kuwaombea wagonjwa. Mnaona? Sasa, ni wangapi wanaojua ambao wamekuwa hapa katika mikutano ijayo, wanaojua ya kwamba Roho Mtakatifu aliyeahidi katika siku za mwisho kwamba huu Ujumbe ungekuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, na Yesu Kristo *ni* yeye yule jana, leo, na hata milele, naye alitoa ahadi ya kwamba angefanya mambo haya katika...ni wasomaji wangapi wa Biblia wanaojua jambo hili, Yeye aliliahidi? Vema.

161 Mnaamini ya kwamba tuko kwenye mwisho wa wakati wa Mataifa, kama ilivyokuwa mwishoni mwa wakati wa Kiyahudi, na wakati wa Kisamaria? Sasa, Yesu alijitambulisha Mwenyewe kama Masihi kwao kwa ishara ya Masihi. Hiyo ni kweli? Kuna mtu anayejua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye alikuwa na ishara ya Masihi? Hakika, hakika Yeye alikuwa nayo.

Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi."

162 Yule mwanamke kisimani alisema, "Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia jambo hili." Mnaona? Na kwa hiyo, kujua siri za moyo wao, kufanya tu jambo lile lile Yeye amefanya daima.

163 Na halafu ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye hakufanya hivyo mbele ya Mataifa? Hakika. Ni wangapi wanaojua Yeye aliahidi *angefanya* jambo hilo wakati wa mwisho? Hakika, Yeye angefanya hivyo, hakika. Vema. Kwa nini? Mungu anapoitwa jukwaani . . . Sasa, sikilizeni ninyi wasomaji wa Biblia, sikilizeni hili, weka imani yako katika Neno la Mungu, kwa kuwa wakati Mungu anapoitwa jukwaani kufanya uamuzi, hawezi kufanya uamuzi mwingine wowote, bali inambidi kudumu na uamuzi Wake wa kwanza. Ni wangapi wanaojua hilo? Maana Yeye hana kikomo, kila uamuzi ni mkamilifu, haimbidi kufanya maamuzi mawili. Kama alifanya uamuzi mwingine, basi uamuzi Wake wa kwanza haukuwa sahihi, kama akiubadilisha. Kwa hiyo wakati Mungu anapofanya jambo lolote katika Biblia hana budi kulifanya tena, la sivyo alikosea alipolifanya mara ya kwanza.

164 Kwa hiyo kama Yeye alijitambulisha kama Masihi kwa ishara ya Masihi, nabii Masihi, halafu kwa Wayahudi, kwa Wasamaria, na kuwaahidia Mataifa, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile.

165 Sasa, ni wangapi wameona hilo likitukia? Hebu tuone mikono yenu nipate kujua. Vema. Loo, nadhani kila mtu. Ni wangapi kamwe hawakuliona likitukia? Hebu tuone mikono yenu. Hawajawahi kuliona, inueni, kamwe hamjawahi kumwona Mungu akifanya jambo kama hilo, akisimama jukwaani? Au hujawahi kuwa kwenye mmoja wa mikutano hii hapo kabla, hujawahi kuona ishara ya Masihi? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa, hamjawahi kuliona. Wachache tu, naam, wageni wengine huko nyuma. Vema.

166 [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Wasemaje? Wasemaje? Naam, katika muda mfupi tu.) Vema, wanafikiri wanaweza kuwapanga hao wengine mstarini. Ishirini na sita. Kadi ya maombi C, ishirini na sita. Ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini, thelathini, thelathini na moja.

167 (Aisee, kuna watu wanaozungumza Kihispania hapa usiku wa leo? Watu hawa wanazungumza Kihispania?) Sijui ni nini huenda hiyo . . . Kuna kadi nne, tano, sita ambazo hazipo ambazo huenda zikawa ni za wanaozungumza Kihispania.

168 Vema, thelathini, thelathini na moja, thelathini na moja. Vema, thelathini na mbili. Hiyo ni kweli. Thelathini na tatu. Njoo moja kwa moja hapa. Thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane. Hapo tunakuja. Thelathini na tisa, thelathini

na tisa. Moja kwa moja huku, njoni huku. Thelathini na tisa, arobaini, arobaini na moja, -mbili, -tatu, -nne. Arobaini na moja, -mbili, -tatu, -nne. Vema, huko nyuma, naam. Arobaini na nne, arobaini na tano, arobaini na sita, arobaini na saba, arobaini na nane. Sikuona arobaini na nane. Arobaini na nane, arobaini na tisa, arobaini na tisa. Arobaini na tisa, sikuiona. Kadi ya maombi C, arobaini na tisa. Vema. C, hamsini. Ni nani aliye na kadi ya maombi C, hamsini? Vema. Sasa tunawapanga mstarini. Sasa, sasa, hizo ndizo kadi zote za maombi.

169 Sasa. . . [Ndugu mmoja anasema, "Mwanamke huyu hapa anahitaji usaidizi, Ndugu Branham."—Mh.] Vema, wakati utakapowadia, wakati utakapowadia watamsaidia huyo mama. Nawaambia, wakati utakapowadia kwangu kumwombea, nitashuka tu nije hapo na kumwombea, umeketi papo hapo madhabahuni. Namba yake ni ipi? Arobaini na nane. Vema, nikumbushe sasa, Ndugu Jack, wakati ikifikia arobaini na nane niende hapo, kumwombea huyo mama. Vema.

170 Sasa, sasa, ninyi wengine hapa ndani msio na kadi ya maombi, ambapo kadi zote za maombi ziko mstarini, sasa, sasa, mnaotaka Yesu awaponye, inueni mikono yenu, msio na kadi za maombi. Vema.

171 Sasa, ninataka kuwanukulia Andiko fulani. Kulikuwa na mwanamke, tunaenda, tutasema tu, wakati mmoja, mwanamke ambaye hakuwa na kadi ya maombi katika Biblia, naye akasema, "Ninamwamini Mtu huyo, na kama tu ningeweza kugusa upindo wa vazi Lake nitakuwa mzima." Mnaijua hiyo hadithi? Vema. Ilikuwaje? Akajipenyeza katikati ya umati, hata akagusa upindo wa vazi Lake.

172 Sasa, kuna mtu yeyote aliyewahi kuona joho la Kipalestina? Linapwaya kabisa, lina vazi la ndani, kuzuia mavumbi kwenye viungo. Nalo vazi la Kipalestina. . . kama angegusa upindo wa koti langu, nisingeuhisi, kama angegusa miguu ya suruali yangu namna *hiyo*, ama sijafu ya suruali yangu nisingeuhisi, vipi kuhusu vazi kubwa linalopwaya namna *hiyo*?

Kwa hiyo, Yesu akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

Ndipo Petro akamkemea, akasema, "Bwana, wote wanakugusa. Kwa nini unasema jambo kama hilo?"

Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu."

173 Nguvu zilitoka. Hiyo ni kweli? Naye alifanya nini? Aliangalia kwenye kusanyiko mpaka akamwona maskini mwanamke huyo, na kumwambia kutokwa kwake na damu kulikuwa kumekwisha, imani yake ilikuwa imemwokoa. Ni wangapi wanaojua hilo?

174 Sasa, hivi usingetaka kumgusa Yeye? Vema, inawezekana kwamba unaweza kumgusa? Je, Yeye ni Kuhani Mkuu sasa anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Vema basi,

kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetendaje sasa? Kama alivyofanya wakati huo. Hiyo ni kweli? Sasa, wewe mguse Yeye uone kama anatenda hivyo, hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Loo, hilo si ni zuri sana, unapolileta Neno la Mungu kwenye shindano la kuamua?

175 Sasa, kama Yeye alisimama hapa amevaa suti hii, nawe ukamwendea ukisema, "Ee Mwalimu, Bwana, Ee Mwalimu, ninaomba ya kwamba utaniponya."

Unajua kile Yeye angesema? "Mtoto wangu, tayari nimefanya hivyo. Hivi huniamini Mimi?"

Unaweza kusema, "Bwana, hebu nione kama una makovu mkononi Mwako."

Mtu yeyote angeweza kuwa na makovu mkononi mwake.

"Hebu nione kama una makovu ubavuni Mwako."

176 Niliyapata mahali farasi aliponirushia. Mbona, mimi. . . Hakika. Sasa, ni—nina lingine *hapa* ambapo nilipigwa risasi kwa bunduki, bunduki ilifyatuka nilipokuwa mtoto, bunduki ya jamaa mwingine ilinipiga risasi ubavuni. Lakini hilo—hilo halimaanishi ya kwamba ungekuwa Masihi, la. Lakini Maisha ya Masihi yangekuwa ni Roho wa Masihi katika Kanisa Lake. Sasa, haidhuru angeiweka juu yangu kiasi gani, hana budi kuiweka juu yako pia, maana hatuwezi kufanya kazi kwa utengano, hatuna budi kufanya kazi pamoja.

177 Yesu alienda mahali fulani akidai Yeye alikuwa ni Masihi, wala matendo mengi makuu asingeweza kufanya, kwa sababu gani? Kutokuamini. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama humwamini, hana njia ya kufanya kazi; kama utamwamini, Yeye ataingia moja kwa moja katika mwili wako, Masihi atakuja. Amina. Yeye ni Mungu yeye yule aliye katika mwili. Mnaamini hilo?

178 Sasa, katika mstari huu wa maombi, ninyi nyote mlio kwenye mstari huu wa maombi, ni wangapi wamekuwa kwenye mistari ya maombi, ambao wamekuwa hapa kwenye mikutano mingine na kumwona Mungu jinsi anavyofunua siri, na kadhalika? Inueni mikono yenu, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi. Vema. Sasa, kama nisipowaambia neno moja, niombe tu, mnaamini ya kwamba Mungu atafanya hivyo? Mnaamini? Mtaamini, bila kuona? Na—na—najua kile unachohisi, ninaweza tu kukihisi. Mnaona? Naweza kulisema jambo hilo.

179 Vema, ninyi huko nje msio na. . .Hebu tufanye mstari wa upambanuzi *hapa* nje, bila kadi za maombi. Wale wasio na kadi za maombi wana upambanuzi, na hebu huyu, *hawa* wapite kusudi mpate kuona ya kwamba Malaika wa Bwana yupo hapa.

180 Sasa, kama Nguzo hiyo ya Moto iliyokuwa pamoja na ninii, iliyokuwa kwenye kichaka kilichowaka moto katika wakati wa Musa. . .Nguzo ya Moto iliyokuwa katika kile kichaka

kilichowaka moto katika wakati wa Musa wakati ilipofanyika mwili, ni wangapi wanaoamini ya kwamba huyo alikuwa ni Kristo? Alisema, "Musa asijakuwako. . . Ibrahimu asijakuwako MIMI NIKO." Mnaona? Vema. Sasa, ile Nguzo ya Moto iliyokuwa nyikani, wakati ilipofanyika mwili, tunajua ilifanya hivyo, sivyo? Na sasa, je, Yeye ni Kuhani Mkuu usiku wa leo anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Vema. Iweni tu na imani na mwamini Mungu, na Mungu ata—atawajalia hilo.

181 Sasa, kila mmoja wenu inamisha tu kichwa chako kwa utulivu, na uanze kuomba, kila mmoja wenu. Msifadhaike, msishikwe na mpagao, bali aminini tu ya kwamba Yesu Kristo yupo hapa. Kama una haja Naye, amini tu.

182 Loo, ni ajabu jinsi gani! Yesu mwenye huruma! Sasa, nimezungumza habari Zake, nikanena Neno Lake, je, sasa Yeye atalitimiza Neno Lake? Vema, hivyo tu. (Umeufanyiza mstari wako wa maombi, sivyo, Billy? Hebu kidogo, hebu kidogo.) Ninataka upambanuzi uwe *huko* nje. Laiti Mungu angaliujalia tu mara nyingine tena!

183 Vema, inueni vichwa vyenu. Nitazameni, sasa, kama tu vile Petro na Yohana walivyopitia kwenye mlango uitwao Mzuri, niaminini, kama mtumishi Wake. Shikilia mateso yako niani mwako, na useme, "Mungu, ninaumwa na *ninii*, unirehemu." Ninyi nyote, msifikiri kwamba mmepita uponyaji, hamjapita. Ni rahisi tu Kwake kuwaponya, kama ilivyo kwa mtu mwingine yeyote, iweni tu na imani.

184 Laiti ningaliweza kumponya kila mmoja wenu, ningefanya hivyo. Siwezi kufanya zaidi ya yale ninayoona yakiendelea. Ninaangalia ile Nuru, ilikuwa hapa sekunde moja tu iliyopita, ikaondoka ikaenda *hivi*, nami siioni sasa, iko nje ya jukwaa wakati huu.

185 Naam, maskini mama huyo hapo aliyetia mkono wake kinywani mwake, akiugua ugonjwa huo wa kibofu nyongo, amini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo anakuponya. Ulikuwa na imani zaidi ya ulivyodhania ulikuwa nayo.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

186 Ndugu uliyeketi papo hapo, usiogope, utakuwa mzima. Na kama utaamini kwa moyo wako wote, mtu huyo unayemwombea, ambaye aliangukiwa na farasi yule, ataamka, kama utaamini. Unaamini? Unaamini? Vema, amini, hakuna lisilowezekana.

187 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Aligusa nini? Yuko futi arobaini kutoka kwangu. Alifanya nini? Alimgusa Kuhani Mkuu. Imani yake ilirudi nyuma, nami nikaishika. Amina. "Kama unaweza kuamini!"

Unafikiri Mungu atakuponya hiyo mishipa iliyovimba?

Hilo si lilikuwa zuri sana?

188 Maskini dada, aliyeketi pale mwishoni mwa safu, unataka Mungu akupe mtoto, sivyo? Maskini mama uliyevaa nguo ya kijani kibichi. Mwamini Mungu, nawe utamkumbatia mwanao uliyemwomba.

189 Waulize hao watu. Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ni mgeni kwangu. Kama… Hatufahamiani, mama, yeyote yule aliyekuwa hapo aliyeitwa? Kama hatufahamiani inua mkono wako, naam, inua mkono wako ili watu waone. Waligusa nini? Kuhani Mkuu. Sasa mnaamini? Sasa wewe gusa. Wewe fanya mguso wa namna ile ile, ninakupa changamoto, katika Jina la Kristo, kufanya hivyo.

Sasa tutawaombea wagonjwa.

190 Hiyo imekugusa? Unaamini ya kwamba mimi ni mtumishi Wake, kwa moyo wako wote? Sikujui. Wewe ni mgeni kwangu, kusudi tu watu waone kama watu hawana kadi za maombi, ama wana kadi za maombi haijalishi. Sasa, mnajua kuna namna fulani ya upako hapa. Hiyo ni kweli? Mnajua ya kwamba ni—ni…Kitu fulani kinahitaji zaidi ya—ya mwa—mwa—mwanadamu kufanya jambo kama hilo. Inahitaji Mungu, sivyo? Naam, hakika inahitaji. Unaamini kwamba Mungu angeweza kuniambia sababu yako ya kusimama hapa? Ambalo lingeninii…Unajua Yeye angeweza, hilo ni sawa. Vema. Kama utaamini…Naona umetiwa uvuli, naam, kitu cha kutisha sana, nawe umetiwa uvuli.

191 Na hiyo ndiyo sababu niliangalia kote, upako ukiwa juu yangu. Nisingeweza kumpitisha kila mmoja wa hao watu kwenye mstari huo, ningeanguka hapa kutoka kwenye jukwaa hili, dhaifu sana sasa. Mnaona jinsi matone ya jasho, yanavyosimama? Mnaona? Nisingeweza kufanya hivyo, kwa sababu kama Yeye alihisi udhaifu kutokana na mtu mmoja kumgusa, vipi sasa wakati inambidi kutenda kazi kupitia kwa mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Mnaona? Na huyo alikuwa ni Mungu aliyetiwa mafuta. Unaona?

192 Mwili Wake mtakatifu tu, uliozaliwa na bikira ambao Mungu alikuwa akifanya kazi kuupitia, ulimfanya dhaifu, vipi kuhusu mimi mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Kwa sababu Yeye alisema, “Mengi kuliko haya mtafanya. Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya, na mengi kuliko haya.” Inasema *kubwa zaidi* katika King James lakini…

Unasema, “Kwa nini unanizungumzia, Ndugu Branham?”

193 Ninajaribu kuwasiliana na roho yako, kama tu Yeye alivyozungumza na yule mwanamke kisimani. Hiyo ni kweli. Ninaweza kukwambia sasa, unaugua wasiwasi mwingi kupita kiasi, una ugonjwa wa moyo, pia. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama hiyo ni kweli inua mkono wako, ili watu wapate kuona hilo.

Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Vema, Mungu yeye yule anajua kitu kiki hiki ndicho shida yako. Unaona? Hilo linatosha tu.

194 Ninaendelea kuhisi hilo kila usiku, mara kwa mara, mtu fulani anasema, “Anabahatisha hilo.”

195 Sibahatishi hilo. Ningewezaje kubahatisha hilo? Sasa, msiyawazie mambo hayo, maana ninayashika papa hapa. Mnaona? Hilo linauzuia mkutano wote. Hapa, hebu tuone kama tulikuwa tukilibahatisha.

196 Wewe ni mtu mzuri. Sasa, nisingeweza kubahatisha hilo, sikujui, sijawahi kukuona, hatufahamiani kabisa. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli. Vema, bwana, hiyo ni kweli. Sasa, sijui yale nimekwambia, njia pekee nijuayo ni kuchukua kanda hiyo.

197 Hebu niwasiliane na roho yako tena. Unaona, wewe ni mwanamke, mimi ni mwanamume. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwenye lango. . .kwenye kisima huko Samaria. Lakini sisi, tukiwa Wakristo, mnaona, na Roho wa Mungu akiwa katikati yetu, sisi ni ndugu na dada, basi kuna Mungu wa Mbinguni hapa anayejaribu kutenda kazi kupitia kwangu, kama *hiki* tu—kitu *hiki*, ha—hakijui la kusema, hakiwezi kusema lolote, wala mimi nisingeweza kuwaambia. Sina budi kuzungumza kupitia *hii* ili kuifanya sauti ipitie ndani yake, vema, Yeye hana budi kunena kupitia kwangu kuniambia kuna shida gani.

198 Mnaliona, enyi wasikilizaji? Mnaona? Mnaona? Sasa, ninajitolea tu, nina karama tu kutoka kwa Mungu kujitolea, sijui atasema nini. Kama anaweza kukwambia yale yamekuwako, hakika ungeweza kuamini, kama Yeye angekwambia yale yatakayotukia.

Sasa, mtu fulani asema, “Vema, hebu tuone kama Yeye atakwambia yaliyokuwako.”

199 Mungu aturehemu ili watu waweze kuona na kuelewa, ombi langu.

200 Ninataka tu. . .Sikusudii, kuyachimbua maisha yako, bali ninataka tu kuona kama Mungu atayasema, kusudi hawa watu waone kitu ambacho. . .Sitamwomba tena, kama Yeye, katika mkutano huu usiku wa leo, kama angelijalia tu litendeke.

201 Naam, ninaliona sasa, ninamwona akitetemeka, akienda dirishani, anashikwa na wasiwasi sana, hasa sana jioni, mara baada ya kazi, naye ana ugonjwa wa moyo. Hiyo ni kwe-. . . Loo, jamani! Kuna jambo lingine, naam, hili hapa jambo ambalo limekuwa: Ni upasuaji wa namna fulani, kansa kwenye titi, nawe unahofu kwamba sehemu yake ingali mle. Hiyo ni kweli. Naam, ubavuni mwako. Mnaona, nilikuwa nikielekeza kwenye mkono wangu wa kushoto, kwa hiyo haikunibidi kuninii. . .Naam.

202 Nawe umekuwa na shida zaidi, umempoteza mume wako hivi majuzi tu. Hiyo ni kweli. Hayo ndiyo yametukia? Unaamini

Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani, yeye yule anayejua Simoni Petro alikuwa ni nani, na kadhalika? Bibi Babb. Sasa nenda ukiamini, yote yatakwisha. Amina.

203 Sasa, kama nikikuwekea tu mikono, kuna *Kitu fulani* kinachotia mafuta hapa, sivyo? Kama nikikuwekea mikono, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya."

Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada yangu na kuomba, wakati upako huu ukiwa hapa, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Nenda, amini sasa kwa moyo wako wote.

Kama nikiweka mikono juu yako, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya? Kanisa zima linakuombea.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Kuwa tu na imani, na uende ukiamini kwa moyo wako wote.

204 Sasa, unajua ninajua shida yako, bali si lazima niiseme, sivyo? Maadamu ninakwambia moyo wako... Loo, endelea, kuwa... Nimekwisha kusema...?... upako huo uko juu yangu.

205 Sasa, unajua ninajua shida yako. Hiyo ni kweli? Kama nikikwambia, itakusaidia? Ni lipi lingekuwa kubwa mno kwangu kukuwekea mikono, ama kukwambia shida yako? Kukwambia shida uliyo nayo. Vema. Unasumbuliwa na wasiwasi, sasa ondoka jukwaani, ukawe mzima.

(Sijui kama nijitikise nitoke kwake au la. Itawabidi kusimamisha mstari wa maombi, mnaona, nisipofanya hivyo. Hiyo hapo tena.)

Unaamini ugonjwa wako wa mgongo utapona? Nenda ukiamini kwa moyo wako wote.

206 Sasa, unajua Mungu angeweza kuniambia shida yako, na kama angeniambia, ingekusaidia? Vema. Ondolea mbali maskini pumu hiyo, endelea, na uamini kwa moyo wako wote...?...

(Siwezi kujiondoa kwake, kwa namna fulani...?... Niombeeni tu.)

Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Moyo wako utakuwa sawa, nawe utapata afya. Vema. Nenda ukiamini kwa moyo wako wote...?...

207 (La, hiyo ni sawa.) Sasa, omba tu na uamini kwa moyo wako wote. Sasa, Yeye anajua shida ya hao watu. Sasa, mnaamini? Sasa, iweni tu na imani, msiwe na shaka. Sasa, kama kila mmoja wenu ataamini, na kukubali tu uponyaji wako, kwa uchaji, mahali ulipo, kubali tu uponyaji wako! Sasa iweni na kicho kabisa. (Iko tena.)

208 Sikujui, sijui lolote kukuhusu. Nadhani hatujawahi kuonana maishani mwetu, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako. Mahali pengine tu kama

Bwana wetu alipokutana na yule mwanamke kisimani wakati mmoja, akazungumza naye. Alipata kujua shida yake ilikuwa ni nini, ndipo basi akamwambia shida yake. Naye akasema Yeye alikuwa ni Masihi. Kama angeweza kukwambia jambo lile lile kupitia kwangu, ungeamini ya kwamba Yeye angali ni Masihi? Unaamini kwa moyo wako wote?

209 Nilitaka tu kukuuliza hilo kwa sababu fulani. Umekuwa na ajali mguuni mwako, ilikuwa, ikang'oa pia ya goti. Hiyo ni kweli. Halafu mbali na hayo, una ngiri inayokusumbua, nawe una wasiwasi sana. Na jambo kuu sana unalohitaji ni kuyatoa maisha yako kwa Kristo, na kutoka mwenye dhambi, uwe Mkristo. Je, utamkubali kama Mwokozi wako sasa? Unamkubali kama Mwokozi wako? Ninakutangaza kwamba umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo. Nenda na usitende dhambi tena.

210 Hebu na tuseme, "Mungu asifiwe," kila mtu. Hebu tumwabudu tu kwa muda kidogo.

Baba Mungu, katika Jina la Yesu, mponye dada yangu.

Baba Mungu, anapopitia hapa jalia aponywe, katika Jina la Yesu.

211 Kama ikiendelea itakubidi kutumia mkongojo baada ya kitambo kidogo, bali unaamini ya kwamba Mungu atakuondolea hiyo? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Hiyo yabisi kavu itakuacha, na itoweke.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe.

Naam, mama, Mungu akubariki, Dada. Asante, Dada.

Baba yetu wa Mbinguni, ninamwekea mikono mwanamke huyu mpendwa, katika Jina la Yesu Kristo, mponye, Baba. Amina.

212 Baba wa Mbinguni, ninapouinamisha moyo wangu Kwako, ninamwombea ndugu yangu, anapopita naomba aingie chini ya vivuli vya msalaba na aponywe, katika Jina la Yesu.

213 Sasa, kama ningekwambia shida uliyo nayo, ingekusaidia? Kwa sababu unajaribu kuwa kipofu, bali hilo silo linalosababisha jambo hili, kisukari ndicho kinacholisababisha. Na kama utaamini kwa moyo wako wote, kitakuacha. Utaamini? Basi katika Jina la Yesu Kristo nenda, ukaponywe. Amina. Ndivyo hivyo . . . ? . . .

Baba Mungu, katika Jina la Yesu Kristo jalia aponywe. Amina.

Amini.

Baba wa Mbinguni, ninaomba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utaponya . . . ? . . .

214 Sasa, msi—msifikiri ni kwa sababu siwaambii kwamba hiyo . . . Kwa namna fulani ni vigumu kwangu kuiondokea. Mnaona? Lakini na—najua ya kwamba ni—ni sawa, Mungu

analifanya vivyo hivyo tu. Mnaona? Um-hum. Haijalishi, mnaona. Siwezi . . . Kama ukifanya mstari mzima, nilimwambia tu Ndugu Jack aangalie, kama ikizidi kuendelea, ingenibidi kuondoka mstarini, maana inazunguka tu kwangu sasa. Ni wangapi wanaofahamu hilo, Kimaandiko? Mbona, hakika. Unaona ni vigumu kwako . . .

215 Vema, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ama, mtumishi Wake, ninakusudia kusema. Hilo huwakwaza watu wengine. Mimi si nabii, mimi ni mtumishi Wake tu. Mnaona? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba atapata afya? Huh? Ana wasiwasi sana, sivyo? Ana ugonjwa wa moyo, shinikizo kuu la damu, naye hunywa pombe. Nenda, amini, huyo ni mume wako ninayenena habari zake, uwe sawa.

Mwamini Mungu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu.

Huh! Nenda ukale chakula chako cha jioni, uliponywa ukiwa umeketi pale kitini, ugonjwa wako wa tumbo umekuacha.

Ee Mungu, ninaomba, Mungu, utamponya mtu huyu, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe.

Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu, naweka mikono juu ya mtoto huyu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Usiogope sasa, itakuwa sawa . . .?. . .

Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya yabisi kavu, na kumpa afya, na wasiwasi, na kadhalika, ninaomba ya kwamba atakuwa sawa, katika Jina la Yesu.

Baba, ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende, na aponywe. Amina.

Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu na kumpa afya, ninapomwekea mikono, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, mwanangu.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende akaponywe. Amina.

Iweni na imani sasa, msiwe na shaka.

Baba yetu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ukipita, kama, usipitie kama ni mimi, bali chini ya msalaba, unaona.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe. Amina.

Loo, usiwe na shaka.

Katika Jina la Yesu, Baba, ninaomba ya kwamba utatujalia baraka hii . . . ? . . .

Mungu awabariki.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, Dada. Unaamini hilo? Uwe na moyo wa ushujaa. Unaona? Sasa, unajua ninajua shida ni nini, bali nenda ukiamini, kwa vyovyote vile. Unaona?

216 Unataka niseme kitu. Kama nitakwambia yaliyo moyoni mwako, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utaamini? Shida moja uliyo nayo, unasumbuliwa na wasiwasi. Hiyo ni kweli. Una tumbo lenye wasiwasi linalokusumbua. Hilo ndilo unalotaka niombee. Hiyo si ni kweli? Umekuwa nao maishani mwako mwote. Nakwambia, una mzigo moyoni mwako. Je, Mungu anaweza kuniambia mzigo wako ni nini? Wokovu wa baba na mama yako, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

Ninakujua, Dada mpendwa.

217 Ee Bwana Mungu, wakati upako wa Roho Mtakatifu, mwanamke huyu amekuwa mkarimu sana kwangu, ninaomba ya kwamba utampa shauku yake usiku wa leo. Mjalie mambo haya yote ambayo ameomba, Baba, na hasa kwa ajili ya familia. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Unajua ninalomaanisha. Vema.

Baba yetu uliye Mbinguni, Litukuzwe kwa Jina Lako, jalia uponyaji wa ndugu ye—yetu wa thamani, katika Jina la Kristo.

Njoo, ukiamini, usiwe na shaka.

Mungu akubariki, ndugu, amini sasa.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamwekea mikono, wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwapo, katika Jina la Yesu na aponywe.

Baba yetu, tunapohisi mitetemo ya mwanamke huyu mwema, ninaomba, Baba, ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Njoo, ukiamini sasa, usiwe na shaka.

218 Dada, angalia tu maombi yanayopaa juu kwa ajili yako, angalia kundi hili zuri la wahudumu hapa, hili ni Kanisa la Mungu aliye hai, unaona.

219 Baba yetu, tunaomba ya kwamba utamponya, wakati kwa imani tunaweka mikono yetu juu yake katika kuyathibitisha Maneno ya Yesu Mwenyewe, Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

"Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa yule, na Mungu atamwinua."

220 Baba wa Mbinguni, pamoja na kuomba kwa bidii kwa wenye haki, wala sisi si wenye haki, bali tunakubali haki ya Bwana wetu, ninaomba maombi haya kwa ajili yake, na kuyawasilisha Kwako kwa niaba yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, Dada. Nenda ukiamini sasa.

Ugonjwa hatari sana uliopo, ugonjwa wa moyo, bali Mungu ndiye Mponyaji wa ugonjwa wa moyo. Hiyo si ni kweli? Unaamini. . .?. . .

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki ndugu yetu na kumponya. Tujalie, Bwana, ninapomwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu.

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe, ninaomba, Baba, ya kwamba utatujalia uponyaji wa ndugu yangu. Amina.

221 Baba Mungu, ninapomwekea mikono maskini mwanamke huyu, ninaomba kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba utamponya na kumfanya mzima kabisa. Amina.

Usitie shaka, njoo tu ukiamini.

222 Bwana Yesu, kwa upole na rehema, Bwana, anamleta huyo mtoto, nami ninawawekea mikono yangu na kutangaza baraka za Mungu, jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, Dada.

223 Baba yetu wa Mbinguni, wakati maskini mwanamke huyu mnyenyekevu anaposogea hapa juu akiwa amebeba Neno la Mungu juu ya moyo mwake, ninaomba, Bwana, itaingia mle ndani kabisa, naye atakuwa na imani ya kuamini, katika Jina la Kristo. Amina.

Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba rehema za Mungu juu ya huyu, dada yetu. Nguvu za Mungu na zimponye na kumpa afya, katika Jina la Yesu Kristo.

224 (Hiyo ni nini? Vema, bwana.) Nitawaomba watu hawa walioketi hapa ambao. . .ingawa hawana kadi za maombi, lakini wako kwenye viti hivi vya magurudumu, hebu nyote mwinamishe vichwa vyenu na kuomba pamoja nami kwa muda kidogo tu, kila mtu, huku nikienda na kuwawekea mikono. [Ndugu Branham anawaombea wale walio kwenye viti vya magurudumu kwa dakika tatu na nusu, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . .?. . .

225 Sasa, ninyi mlio-. . .mliokuwa hapa bila kadi, na, niliwaombea watu hawa kwenye kiti cha magurudumu, wala hawakuwa na kadi pia, lakini wana wakati mgumu sana kufika mkutanoni. Mimi. . .Je, nilimwombea maskini jamaa huyu hapa? Mungu akubariki, Ndugu. Nakutakia heri. [Ndugu Branham anamwombea huyo mvulana, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] Baba yetu wa Mbinguni. . .?. . .

226 Tulizoea kuimba ule wimbo mdogo:

> Ombeni, ombeni, ndiyo njia pekee
> Kufikia mahali pa juu zaidi;
> Ombeni, ombeni, maombi ya imani
> Yatashusha baraka za Mungu.

Hiyo ni kweli? Je, ninyi nyote mnamwamini Mungu?

227 Samahani, nafikiri mstari wa maombi umekwisha. Huyu tu? Vema. Huyu—huyu ndiye yule mama mwingine? Vema. Sasa, wewe ni . . . Wangapi wanaamini?

Mama huyu, sikujui, sijawahi kukuona nijuavyo mimi. Hatufahamiani.

228 Sasa, kila mtu hapa nje jengoni, hebu mwanamke huyu awe mfano kwako. Sisi hapa, tembea tu moja kwa moja uje upande huu, Dada. Simjui mwanamke huyu, sijawahi kumwona. Hatufahamiani kabisa, nijuavyo mimi. Lakini kama Roho Mtakatifu ataniambia shida yake, ama kilichomleta hapa, huenda ikawa yeye ni mgonjwa, labda yuko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, labda yuko hapa kwa ajili ya matatizo ya nyumbani, matatizo ya kifedha, mambo ya kanisa, hali ya kiroho, sijui. Hiyo ni kweli, simjui huyo mama, Mungu anamjua.

229 Lakini sasa ili ninyi watu daima mpate kujua ya kwamba Yesu Kristo, yuko mbele zenu, akifanya thibitisho lisiloweza kukosea la Neno Lake, hebu nizungumze na huyu mwanamke kwa muda kidogo tu, huku nimejitolea kwa Roho.

230 Sasa, ninyi niliowaombea, na kuwawekea mikono kwenye viti hivi vya magurudumu, kama huna imani ya kutosha kusimama na kutembea, hilo lisikusumbue, wewe kuwa tu na imani ndogo kama mbegu ya haradali, na uishikilie moja kwa moja, na iendelee tu kukupeleka mbele moja kwa moja. Unaona? Sasa, Ibrahimu alipewa ahadi ya Mungu, na kwa muda wa miaka ishirini na mitano alingojea ahadi hiyo kutimizwa. Hiyo ni kweli? Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; alikuwa na nguvu akimpa Mungu sifa. Sasa, tunajua ya kwamba Mungu angali anabaki Mungu.

231 Sasa, kama mwanamke huyu hapa, akienda Mbele za Bwana Yesu Kristo usiku wa leo, hebu tuseme yeye ni mgonjwa, naye akaenda Mbele za Bwana Yesu, naye . . . Yeye *yuko* Mbele za Bwana Yesu, si wewe, si mimi, bali Roho aliye hapa. Mnaona? Yeye ni Mzabibu, sisi ni matawi. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua mzabibu hauzai matunda? Matawi huzaa matunda kwa kuwa yanatiwa nguvu na mzabibu. Hiyo ni kweli? Sasa angalieni kwa makini na msikilize. Sasa, kama angesimama hapa Mbele za Bwana Yesu . . .

232 Jambo fulani lilitendeka kwa mvulana huyo pale basi. Hebu nikwambie kile ninachotaka ufanye, ninataka uchukue kamba na kuifunga kwenye hicho kichwa kilichojawa maji, unaona,

usiku wa leo, na ufunge fundo kwayo. Kisha kwenye usiku wa mwisho wa mkutano, kesho kutwa usiku wewe, kesho usiku utafunga fundo lingine, kesho yake usiku fundo lingine, kisha uniletee hiyo kamba, na kuiweka hapa juu ya hili *hapa*, ikithibitisha ni Mungu aliye juu ya mvulana huyo. Nawe utaona hicho kichwa kinasinyaa kiasi gani kati ya sasa na wakati huo. Amina. Hilo ni kwamba mpate kujua.

233 Sasa, sababu ya mimi kufanya hivyo ni kuwa na imani yake, unaona, huna budi kuwa na kitu fulani kwa ajili ya imani yako. Unaona? Kama hutashuku, litatukia. Sasa, angalieni, ninataka ufunge kamba yako, ufunge fundo dogo ndani yake, kisha uweke kamba iyo hiyo, kesho usiku, baada ya ibada, ufunge fundo lingine dogo, kinasinyaa kiasi gani, halafu kwenye usiku wa mwisho ufunge fundo lako nililozungumzia kanisani, kisha uiweke hapa jukwaani, uikate, na unionyeshe ni kiasi gani kilipungua kati ya sasa na wakati huo, tutaona.

Sasa, mnaona, marafiki, mnasema, "Unafanya nini, Ndugu Branham?"

234 Ninajaribu kujirudisha mahali fulani kidogo tu, mnaona, ili niweze kuzungumza nanyi kwa muda kidogo tu. Ninaangalia huko nje na kuona tu, kana kwamba ninyi nyote ni kundi moja kubwa, lililonyong'onyea sasa. Mnaona? Lakini ninajaribu kuwafanya mwone ya kwamba ndugu yenu, mimi, ndugu yenu, kamwe hana uhusiano wowote na jambo hili, ni Mungu akithibitisha Neno Lake, ahadi Yake, ambalo alisema angefanya.

235 Sasa, msiogope hilo. Kama ningeweza kuisikia Sauti Yake ikinena usiku wa leo, Yeye angesema hivi: "Jipeni moyo; ni mimi; msiogope." Kwa kuwa Yeye ni yule yule jana, hivyo ndivyo alivyofanya jana, ni leo, itakuwa milele. Mnaamini hilo?

236 Sasa, mnaona, ili kwamba mjue ya kwamba si kadi za maombi, ama kitu fulani, mtu fulani, ama katika kiamshakinywa cha wahudumu. Na kwa siku tatu usiku sasa, ibada tatu hatujakuwa na kadi ya maombi. Na je, amefanya ibada zingine bila kadi za maombi, kama tu alivyofanya usiku wa leo na kadi za maombi? Kadi za maombi zinawaweka tu mstarini, kusudi tusipiganie mahali pa mmoja na mwingine, mnaona, kusongamana sana mahali pamoja.

237 Sasa, Dada, samahani, ninaendelea kusahau hilo. Mimi, sijarukwa na akili, lakini natumaini utanisamehe hilo, sikumaanisha usimame hapa na kukufanya kitu cha kukodolea macho. Sasa, ninii tu . . . Sisi . . . Je, ulikuwa na kadi ya maombi, ama walikupandisha tu hapa? Ulikuwa na kadi ya maombi. Vema. Kwa sababu nilifikiri kama uliweza kutembea kote namna hiyo, isingekuwa sawa na, mwajua, kwa sababu ungeweza kuwa ninii . . . unaona, kwao. Lakini wewe, walikupa kadi ya maombi, ulikuwa mstarini. Vema.

238 Sasa, kama Bwana Yesu, kama hapa, mwanamke na mwanamume tena, kama Yeye anaweza kuniambia jambo fulani ambalo, lililokuleta hapa, ungeliamini? Uko hapa nipate kuyaombea macho yako, una shida ya macho. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Vema, unasema, "Hakika, amevaa miwani."

239 Vema, hebu tuondoe tu hilo njiani. Sasa wewe nitazame na uamini. Unaamini? Sasa, wewe ni . . . Kuwafanya tu watu wajue, sasa, sasa hivi unasikia Roho tamu sana, yenye joto. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako, maana wewe ni Mkristo.

240 Sasa, hivi uliwahi kuona picha ya ile Nuru, ile Nguzo ya Nuru kwenye picha? Tunayo hapa, imechukuliwa kote ulimwenguni, tunazo mumu humu jengoni. Sasa, ni wangapi wamewahi kuiona? Vema, Nuru hiyo imening'inia kati yangu na mwanamke huyu sasa hivi, ninaiangalia moja kwa moja.

241 Sasa, unafikiri Yeye angeweza kumponya mume wako? Yeye yupo hapa, pia. Kama ninaweza kukwambia shida ya mumeo, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Ana kansa ya ngozi usoni. Hiyo ni kweli, sivyo? Uh-huh. Vema.

242 Nawe una mpendwa mwingine unayemwombea, huyo ni binti, mpendwa, hawako hapa, ana ugonjwa wa sikio. Hata hawako katika nchi hii, ni huko Georgia. Hiyo ni kweli? Wewe hutoki kwenye mji huu, unatoka kwenye mji unaoitwa J-a- . . . Jasper. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Kennett. Naam, hiyo ni kweli. Nenda nyumbani, ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

243 Weka . . . Wangapi wanaamini? Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na *hao* waaminio." Hiyo ni kweli? Wekeaneni mikono. "Wakiweka mikono . . . " Usijiombee mwenyewe sasa, mwombee mtu uliyeninii . . . Huko nyuma kabisa huko, wekeaneni mikono. Sasa ombeni maombi ya imani.

244 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utawasaidia.

245 Shetani, umeshindwa vita, umefichuliwa, Shetani. Toka ndani yao katika Jina la Yesu Kristo!

61-0123 Msiogope, Ni Mimi
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org